# Nipashe

Jumamosi Julai 20, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579975

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twi... hetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Sababu mbili Lissu kumshtaki Ndugai

UKURASA 3




UKURASA 13

# Zitto ajitosa sakata Kinana, Makamba

• **Ashauri** viongozi wakuu wastaafu kuingilia kati sakata hilo ili... *Endelea ukurasa 2*


## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**12 WATOSWA JKT KISA HOMA YA INI**

VIJANA 12 kati ya 325 walioteuliwa kujiunga na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) mkoani Mtwara, wameenguliwa baada ya kugundulika kuwa...

UKURASA WA 4

**TAASISI YA MENGI YAWATIA MOYO WENYE ULEMAVU**

MDHAMINI wa Taasisi ya Dk. Reginald Mengi iliyoanzishwa kwa ajili ya watu wenye ulemavu, 'Dk. Reginald Mengi Persons with Disabilities Foundation...

UKURASA WA 5

**BENKI YA DUNIA YASAIDIA TANZANIA TATHMINI**

BENKI ya Dunia, kwa kushirikiana na serikali ya Tanzania kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Idara ya Menejimenti ya Maafa, imeendesha mafunzo juu ya


## Bodaboda kortini tuhuma ulawiti

UKURASA 3




UKURASA 2

Jaji Mkuu, Prof. Ibrahim Juma, akizungumza katika mahafali ya 60 ya Shule ya Sheria Tanzania, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Jaji Mkuu ataka dhamana kesi za mauaji, uhujumu

**MICHEZO** **KIDAO: TAIFA STARS ITAFUZU AFCON** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# 12 watoswa JKT kisa homa ya ini

**Na Hamisi Nasiri,** MTWARA

VIJANA 12 kati ya 325 walioteuliwa kujiunga na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) mkoani Mtwara, wameenguliwa baada ya kugundulika kuwa na homa ya ini.

Imelezwa kuwa vijana hao wameenguliwa hatua za mwisho za kujiunga na jeshi hilo baada ya vipimo kubainisha wana ugonjwa huo.

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, wakati akifungua kikao cha Kamati ya Ushauri mkoa jana, alisema vijana 12 kati ya 325 waliofanyiwa usaili kwa ajili ya kujiunga na JKT mkoani mwake wamebainika kuwa na homa ya ini.

Byakanwa alibainisha kuwa kati yao, 10 wanatoka Wilaya ya Nanyumbu na wawili ni wanatoka Wilaya ya Newala.

Alisema wamesikitishwa na taarifa ya vipimo hivyo kutoka kwa Mganga Mkuu wa Mkoa huo kwa kuwa vijana hao tayari walikuwa katika hatua ya mwisho kujiunga na jeshi hilo, lakini kutokana na changamoto hiyo ya kiafya imebidi waenguliwe.

Alisema serikali ya mkoa tayari imeshatoa maagizo kwa Mganga Mkuu wa Mkoa kuwachukua vijana hao na kuandaa utaratibu bora zaidi kuhakikisha wanapata matibabu sahihi ya ugonjwa huo.

"Hili siyo jambo la kufurahisha, vijana hawa kilichowatokea kugundulika na homa ya ini na hapa ukiangalia vijana wengi ni kutoka Wilaya ya Nanyumbu ambayo peke yake ina vijana 10 wamegundulika kuwa na homa hii na wengine wawili ni kutoka Wilaya ya Newala," Byakanwa alisema.

Kiongozi huyo wa mkoa aliitaka jamii kuwa na utamaduni wa kufanya mazoezi mara kwa mara, akiamini kufanya hivyo kutasaidia kuepekana na magonjwa mbalimbali. Mganga Mkuu wa Hospitali ya Mkoa wa Mtwara, Silvia Mamkwe, akizungumza katika kikao hicho, alisema homa ya ini ni ugonjwa ambao hushambulia na husababisha ini kuvimba.

Alisema kuna sababu mbalimbali zinazopelekea mtu kupata ugonjwa huo zikiwamo sumu, pombe, maambukizo na matumizi ya dawa.

"Kuna aina tano za homa ya ini na mtu anaweza kupata maambukizo ya virusi hivi kwa sababu mbalimbali ikiwamo kugusana na damu," alisema.

Mamkwe alisema dalili za homa ya ini zinafanana kwa aina zote za ugonjwa huo na wakati mwingine hutofautiana kati mgonjwa mmoja na mwingine.

Alizitaja baadhi ya dalili za awali za ugonjwa huo kuwa ni pamoja na uchovu, homa, kuharisha, maumivu ya tumbo na mwili kuwa na manjano.

# Zitto ajitosa sakata Kinana, Makamba

**Na Enock Charles**

KIONGOZI Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema kuna haja viongozi wakuu wastaafu kujitokeza kuzungumzia malalamiko yaliyotolewa na makatibu wakuu wastaafu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana na Yusuf Makamba, akidai yamewagusa wadau wengi.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Kinana na Makamba waliandika barua kwa Baraza la Ushauri la Viongozi Wakuu Wastaafu wa chama hicho wakilalamika kuhusu tuhuma za kumhujumu Rais Magufuli zilizotolewa dhidi yao na mtu anayejiita mwanaharakati huru.

Tayari baraza hilo limeshawajibu wawili hao kupitia katibu wake, Pius Msekwa, likieleza kuwa suala lao lilipaswa kushughulikiwa kwa kuzingatia taratibu zilizoainishwa kwenye katiba ya chama hicho badala ya kukimbilia kwao.

Msekwa ambaye ni Makamu Mwenyekiti mstaafu wa CCM, katika majibu hayo pamoja na mambo mengine, alisema kuwa baraza hilo jukumu lake ni kutoa ushauri tu kwa viongozi walioko madarakani na kwamba maamuzi ya masuala mbalimbali yanashughulikiwa na vyombo husika vya chama.

"Mimi naliona kama jambo la kitaifa kwa kuwa ... (alitaja jina la anayelalamikiwa na kina Kinana) amekuwa ni mwiba kwa hali ya usalama wa nchi yetu, amekuwa akituhumu watu mbalimbali.

"Mimi nina taarifa kwamba kilichokuwa kinatengenezwa ni kuonekana mazingira ya kuwa kutakuwa na masuala ya kihaini katika nchi na wanaokuwa 'targeted' (lengwa) ni viongozi mbalimbali nchini," Zitto alidai jana.

Kiongozi wa ACT-Wazalendo huyo alidai ugomvi huo ndani ya CCM ni hatari kwa usalama na utulivu katika nchi, akitahadharisha kuwa usipopatiwa ufumbuzi mapema, huenda ukasababisha madhara makubwa na hata kusimamishwa kwa uchaguzi ujao. "Ugomvi ndani ya CCM ni ugomvi wa kitaifa kwa sababu unapelekea kutengenezwa jambo ambalo ni hatari kwa nchi kwa sababu kukiwa na uhaini, kutatangazwa hali ya hatari, vyama vya siasa vitasimamishwa, baadhi ya vipengele vya katiba vitasimamishwa na uwezekano mkubwa ni kusimamisha uchaguzi," Zitto alitahadharisha.

Zitto (42), ambaye pia ni Mbunge wa Kigoma Mjini, amewahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC).

Kipindi hicho mwanasiasa huyo alikuwa mwanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) alichokihama Machi 19, 2015 na kujiunga na chama chake kipya cha ACT-Wazalendo.



Wahitimu wa shule ya Sheria Tanzania (kutoka kushoto), Hamza Hilal, Mohamed Mpochi na Abia Richand wakipongezana wakati wa sherehe ya mahafali ya 60 ya shule hiyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Jaji Mkuu ataka dhamana watuhumiwa kesi mauaji

**Na Beatrice Shayo**

JAJI Mkuu wa Tanzania,Ibrahimu Juma, amesema mahakama inapendekeza kesi zote zikiwamo za mauaji ziwe na dhamana kwa watuhumiwa ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kukabiliana na msongamano wa wafungwa na mahabusi magerezani.

Kiongozi huyo wa mahakama aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akiwaapisha mawakili 720. Alisema suala hilo linawenzaka kama ilivyo katika nchi ya Kenya ambayo dhamana inatoka kwenye kesi zote zikiwamo za mauaji.

"Sisi kama mahakama tuna mapendekezo tuwe kama Kenya, makosa yote yapewe dhamana. Mahakama iachiwe haki ya kusimamia dhamana, yaani sheria isifunge dhamana, hatutakuwa na hilo tatizo (msongamano wa wafungwa na mahabusi). Kenya tumeona mahakama inatoa dhamana kwenye kesi za mauaji, hilo linawezekana kabisa," alisema.

Kuhusu masharti ya dhamana, Jaji Juma alisema wanapendekeza yalegezwe, akieleza kuwa wananchi wengi sasa wana vitambulisho vya taifa, hivyo kuna haja vitumike kama dhamana badala ya kumtaka mwananchi kuonyesha mali.

Alisema msongamano uliopo umetokana na upungufu katika sheria za nchi, akibainisha wengi wa wanaonyimwa dhamana ni wanaotuhumiwa kwa kesi kubwa zikiwamo za mauaji, uhujumu uchumi, dawa za kulevya na ubakaji.

"Kwa bahati mbaya kesi hizo zina adhabu kubwa na vilevile upelelezi unachelewa kukamilika, nadhani watu wa kulaumiwa hasa ni wapelelezi, siyo mahakama na wala siyo mtu mwingine, upelelezi unachukua muda mrefu na sababu wanazozitoa mahakamani kuhusu upelelezi kutokamilika, hazina mashiko," alisema.

Alisema kunapokuwa na kesi ya muda mrefu bila kukamilika kwa upelelezi, sheria inatakiwa kutamka wazi kwamba inapofika wakati fulani kama kesi haijakamilisha upelelezi wake, ifutwe.

"Sheria inatakiwa kutamka, sisi wa mahakama tutaitekeleza," Jaji Mkuu alisema.

Kiongozi huyo wa mahakama pia aliwataka wananchi kubadilisha mtazamo wa kupenda adhabu kali zaidi badala ya kutoa adhabu mbadala.

"Ukisikiliza mijadala ya bungeni, kila mtu anataka adhabu kali miaka 30 ama 15, hizo zote zinachangia magereza kujaa," alisema.

Aliongeza kuwa hata kwenye siasa za nchi nako kuna changamoto zinazopaswa kuangaliwa.

"Mkandarasi akishindwa kutekeleza matakwa ya mkataba, utasikia kamata weka ndani, hizi zote zinachangia, tuache masuala ya kijinai yaende kijinai na masuala yanayohusu mambo ya mikataba yaende kimkataba," alishauri.

SHABIKI MKUU WA TAIFA STARS




SHABIKI MKUU WA TAIFA STARS




# Sababu 2 Lissu kumshitaki Spika Ndugai mahakamani

**Na Romana Mallya**

MWANASHERIA Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu, ametaja sababu mbili zinazompeleka mahakamani kumshtaki Spika wa Bunge, Job Ndugai (pichani).

Lissu (51), ameamua kuchukua uamuzi huo baada ya kiongozi huyo wa Bunge kutangaza kumvua ubunge mtaalamu huyo wa sheria.

Katika taarifa yake kwa umma jana, Lissu alisema hana ugomvi wowote na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) iliyoamua kuitisha uchaguzi mdogo kwenye Jimbo la Singida Mashariki alilokuwa analiongoza, bali Spika Ndugai na uamuzi wake.

Alitaja sababu mbili za kufungua kesi katika Mahakama Kuu ya Tanzania kuwa ni kutaka uhalali wa sababu zilizotolewa na Spika Ndugai kumvua ubunge na kama kiongozi huyo wa Bunge hakuwa na taarifa kuhusu aliko mbunge huyo.

"Tunachoenda kuiomba Mahakama Kuu iamue kama ni halali kwa mujibu wa katiba na sheria za Tanzania kwa mbunge kuvuliwa ubunge kwa sababu zilizotolewa na Spika Ndugai, bila kuulizwa chochote au kupewa fursa ya kujitetea.

"Pili, tutaiomba Mahakama Kuu ijibu swali la kama kweli Spika Ndugai hakujua mahali niliko kwa muda wote huu tangu September 7, mwaka 2017," Lissu alieleza katika taarifa yake hiyo iliyothibitishwa na Mkuu wa Idara ya Habari Mawasiliano Chadema, Tumaini Makene, alipotafutwa na Nipashe jana.



Katika taarifa hiyo, Lissu alisema Mahakama Kuu ikikubaliana na Spika Ndugai, maana yake ni kwamba aliondolewa ubunge kihalali.

"Lakini, ikisema kwamba Spika Ndugai alikuwa anajua niko wapi na alitakiwa anisikilize kwanza kabla ya kunivua ubunge, basi kilichofanyika leo kitakuwa sawa na sifuri.

"Taratibu zote hizi za kufungua kesi zimekamilika kwa kiasi kikubwa. Kilichobakia ni kwa mawakili kumaliziamalizia kupitia nyaraka zote ili twende mahakamani tukiwa tumekamilika," Lissu alieleza zaidi katika taarifa yake hiyo.

Aliongeza kuwa matumaini yao ni kwamba wiki ijayo haitaisha kabla hawajakwenda Mahakama Kuu kufungua kesi hiyo

"Nimekaa kimya sana kwenye

INAENDELEA UK. 8

# Bodaboda kortini tuhuma kubaka, kulawiti wanafunzi kwa vitisho

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

MWENDESHA bodaboda, Boniphace Godfrey (24), mkazi wa Kabarimu mjini Bunda, mkoani Mara, amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Bunda, kwa makosa ya kubaka na kulawiti wanafunzi wadogo wa chini ya umri wa miaka kumi katika maeneo tofauti.

Kwa mujibu wa Mwendesha Mashtaka, Inspekta Jonas Kaijage, mtuhumiwa huyo alitenda makosa hayo kati ya Mei na Juni mwaka huu, katika maeneo ya Kata ya Kabarimu.

Kaijage aliiambia mahakama hiyo mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Kusaga Majinge, kwamba mshtakiwa huyo alikuwa akiwavizia na kuwarubuni wanafunzi hao kwa kuwapa pipi na fedha kidogo, kisha kuwafanyia ukatili huo kwenye nyumba ambazo hazijakamilika kujengwa.

Aidha, Kaijage alidai kuwa mshtakiwa huyo wakati akiwafanyia vitendo hivyo vya kinyama, alikuwa akiwatishia kwamba iwapo wakithubutu kumwambia mtu yeyote atawaua.

Aliendelea kuiambia mahakama hiyo kuwa, matukio hayo yaligundulika baada ya mwanafunzi mmoja kati ya wale wenzake aliyefanyiwa unyama huo kushindwa kuvumilia na kumtaja mshtakiwa huyo kwa wazazi wake, ndipo alipokamatwa.

Upelelezi wa kesi hiyo haujakamika na mtuhumiwa huyo alirudishwa mahabusu hadi Jumanne, kesi hiyo itakapotajwa tena.

Katika tukio lingine, Juma Wambura Marigo (28), mkazi wa Kijiji cha Nyamatoke Wilaya ya Bunda, amehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka mitano jela baada ya kupatikana na hatia ya kumjeruhi kwa kumchoma na kisu begani mwanamke mmoja.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Bunda, Majinge, baada ya kuridhika na ushahidi uliotolewa mahakamani hapo na upande wa mashtaka pasipo kuacha shaka yoyote.

Awali Mwendesha Mashtaka, Inspekta Kaijage, aliiambia mahakama hiyo kuwa mshtakiwa huyo alimjeruhi kwa kisu Rosemary Ngoboko, mkazi wa kijiji hicho, baada ya kuvunja mlango wa nyumba yake na kuingia ndani kwa lengo la kutaka kumlazimisha wafanye naye tendo la ndoa.

Kaijage alidai kuwa mlalamikaji alipokataa, huku akipiga kelele za kuomba msaada, mshtakiwa huyo alitoa kisu alichokuwa nacho na kumchoma sehemu ya begani na kumjeruhi vibaya.

Alifafanua kuwa tukio hilo lilitokea Feb 29, mwaka huu, saa tatu usiku nyumbani kwa mwanamke huyo.

Kutokana na ushahidi uliotolewa mahakamani hapo pasipo kuacha shaka yoyote, Hakimu Majinge, alimuhukumu adhabu ya kifungo cha miaka mitano jela, na pia kutakiwa kumlipa mlalamikaji Sh. 100,000 kama fidia, na kusema kuwa adhabu hiyo itakuwa fundisho kwake na kwa watu wengine wenye nia na tabia kama hiyo.

Kabla ya hukumu hiyo kutolewa, Inspekta Kaijage aliiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa kwa madai kuwa kitendo alichofanya ni cha kinyama, na hakikubaliki ndani ya jamii iliyostaarabika na kwamba adhabu hiyo itakuwa fundisho kwa vijana wengine wenye tabia kama hiyo.

Alipopatiwa fursa ya kujitetea, mshiakiwa huyo aliiomba mahakama kumpunguzia adhabu. Hata hivyo, ombi hilo lilitupiliwa mbali na Hakimu Majinge.

# Ataja kitakachoibeba CCM uchaguzi 2020

**Na Enock Charles**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimeendelea kusisitiza kuwa kina uhakika wa kupata kura zisizopungua milioni 10 katika uchaguzi mkuu wa mwakani kutokana na mtandao mkubwa wa wanachama kilionao kuanzia ngazi ya mashina.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Humphrey Polepole, alisema jana kuwa mikakati ya ushindi ya chama hicho ni pamoja na kuimarisha mtandao huo wa wanachama huku akijivunia kile alichokiita kazi nzuri inayofanywa na Mwenyekiti wa chama hicho, Rais John Magufuli.

"Viongozi wa mashina ndiyo wanahakikisha ushindi wa CCM kwa sababu hawa ndiyo kiungo kati ya umma na chama chetu, viongozi wa mashina wanakadiriwa kuwa kati ya 230,000 na 240,000.

"Ukichukua mwenyekiti wa shina na kamati yake ile ya watu wanane mara 240,000, wanakuwa zaidi ya milioni moja. Kwa hiyo, tukisema kila kiongozi wa shina atuletee watu wake 10, maana yake tuna kura za uhakika milioni 10," Polepole alitamba.

Alisema chama hicho kina wanachama zaidi ya milioni 10 nchi nzima, hivyo ana uhakika kitaibuka na ushindi wa kati ya asilimia 70 na 90 katika uchaguzi mkuu wa mwakani.

Aliwataka wanachama wa chama hicho kuwakabili wapinzani kwa kuwapa habari za miradi mbalimbali na mambo mengine yaliyotekelezwa na na chama na serikali.

"Iko miradi mingi ya msingi kabisa na kimaendeleo, hizi habari tuziseme tena na tena, mpaka kila mtu anapokuwa anajiwazia mambo yake afahamu miradi hii," Polepole alisema.

TAIFA STARS VS KENYA
JULAI 28, 2019 • UWANJA WA TAIFA

HAIUZWI KWA WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA 18. TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU.

# Taasisi ya Dk. Mengi yawatia watu wenye ulemavu moyo

**Na Romana Mallya**

MDHAMINI wa Taasisi ya Dk. Reginald Mengi iliyoanzishwa kwa ajili ya watu wenye ulemavu, 'Dk. Reginald Mengi Persons with Disabilities Foundation,' Jacqueline Mengi, amewatia moyo watu wenye ulemavu kwa kuwaeleza kuwa wataenzi mambo yote aliyoacha mwasisi wa taasisi hiyo.

Jacqueline aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika kongamano la kuwatangaza mabalozi wa tuzo za I CAN ambao ni miongoni mwa washindi walioshinda mwezi Machi mwaka huu.

Katika kongamano hilo, washindi hao ambao ni watu wenye ulemavu, walijadili na kutengeneza mkakati wa kuendeleza kazi na urithi wa Dk. Mengi aliyouacha katika taasisi hiyo baada ya kufariki Mei 2, mwaka huu.

"Nikiwa mdhamini wa taasisi hii na mjane wa Dk. Mengi, nawahakikishia watu wenye ulemavu, wafanyakazi na mkurugenzi wa taasisi hii, Shimimana Ntuyabaliwe, moja ya jambo muhimu ni kuendeleza yale aliyoacha," alisema.

Jacqueline alimshukuru Rais John Magufuli; Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan; Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa; Spika wa Bunge, Job Ndugai; vyombo vya ulinzi na usalama na viongozi mbalimbali zikiwamo taasisi na mashirika kwa mchango wao wakati wote wa msiba wa Dk. Mengi.

"Kama familia hatuna cha kuwalipa, asanteni sana kwa sababu ukiwa na matatizo ndio utajua rafiki zako ni nani, kwa kweli Watanzania walionyesha kuwa ni marafiki wa Dk. Mengi," alisema.

Pia alitoa pole kwa jamii ya watu wenye ulemavu kwa kuondokewa na baba, mlezi, mshauri na mtetezi wao.

"Ninajua sisi tumeondokewa, lakini nyie mmepata pigo kubwa sana, Dk. Mengi aliwapenda sana, haiwezi kupita siku au wiki bila kuzungumza marafiki zake, ndugu zake ambao ni watu wenye ulemavu, aliwapenda na kuwajali kwa dhati," alisema.

Alisema Dk. Mengi alikuwa na ndoto ya kuona siku moja watu wenye ulemavu wakiondokana na changamoto za umasikini, kutothaminiwa, kunyanyaswa kubaguliwa na kutopewa heshima stahiki.

"Ameacha alama kubwa na funzo kwa jamii ya kutambua na kuheshimu watu wenye ulemavu na hiyo ndiyo heshima ya kipekee itakayodumu kwa miaka mingi ikimwakilisha Dk. Mengi," alisema.

Alisema kutokana na ushauri alioutoa Waziri Mkuu, Majaliwa, wakati wa chakula cha mchana miwili iliyopita, alianzisha taasisi hiyo ya PWD.

Akizungumzia kitabu cha Dk. Mengi cha I Can, I Must, I Will, alisema kazi ya kukitafsiri kwa lugha ya Kiswahili alipewa Mhadhiri Mwandamizi wa Tafsiri na Taaluma za Kiswahili kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Dk. Hadija Jilala.

"Kazi ya kutafsiri kile kitabu chetu cha I Can, I Must, I Will, Dk. Mengi alimpa Dk. Jilala, kipo katika hatua ya mwisho ya kutafsiriwa, Dk. Jilala ni mmoja wa watu wenye ulemavu ambaye ni miongoni mwa mabalozi waliopewa nishani," alisema.

Mkurugenzi wa Taasisi Mtendaji wa PWD, Shimimana, alisema matumaini yao ni kushirikiana na wadau wengine ili kujenga uwezo na kupanua wigo wa taasisi hiyo kuendesha kampeni na miradi mingi mikubwa kwa ajili ya kundi hilo.

Akitoa neno la shukrani, Dk. Jilala alisema kitendo cha kuitwa hapo na kupewa nishani kama mabalozi wa tuzo za I Can, inaonyesha wazi wapo na nia moja ya kuendeleza yale aliyoacha Dk. Mengi.

"Tunajivunia taasisi hii kama ni chombo pekee ambacho kinaweza kuweka alama kubwa ya Dk. Mengi, kama jamii ya watu wenye ulemavu tunatoa pole zetu kwa familia na kuwaahidi wewe ni mama yetu na sisi ni rafiki zako kama ambavyo tulivyokuwa kwa Dk. Mengi," alisema.



Mdhamini wa Taasisi ya Dk. Reginald Mengi kwa ajili ya watu wenye ulemavu, Jacqueline Mengi, akimvisha medali ya kumtambua kama Balozi wa tuzo za I CAN, mwenye ulemavu, Wakonta Kapunda, wakati wa kongamano jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

## Tanroads yatoa angalizo wizi miradi barabara

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

WAKALA wa Barabara Tanzania (Tanroads) umewapa angalizo wananchi wa Mkoa wa Kigoma kuacha tabia ya wizi na kutumia silaha kwenye miradi ya ujenzi wa barabara za lami.

Angalizo hilo lilitolewa na Mtendaji Mkuu wa Tanroads, Mhandisi Patrick Mfungale, jana kwenye ufunguzi wa mradi wa ujenzi wa barabara ya lami katika Kijiji cha Kabingo hadi Kibondo, Kasulu, Buhingwe na Manyovu.

Alisema Barabara hii ya Kabingo, Kasulu, Manyovu na Rumunge hadi Oitaza upande wa Burundi ni sehemu ya mtandao wa barabara za Afrika Mashariki, na ndiyo maana mwakilishi kutoka Burundi alikuwapo kwa ajili ya mradi huo ambao utazinufaisha pia nchi za Rwanda, Uganda na Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (DRC).

Barabara za Kabingo na Kasulu ni kiunganishi cha mtandao wa barabara kwa upande wa magharibi mwa Tanzania.

Alisema mradi huo unatekelezwa kwa fedha za mkopo nafuu kutoka Benki ya Afrika ambayo imeshatoa jumla ya Sh. bilioni 500 na serikali ya Tanzania itachangia Sh. bilioni 58 ya mradi huo kwa mujibu mkataba uliotiwa saini kati yao na Benki ya Afrika.

Mhandisi Mfugale alibainisha kuwa kuna wizi mdogo mdogo kwenye miradi ambapo baadhi ya watu wanaiba mafuta, nondo na mabati, ingawa alisema ni jukumu la mkandarasi kudhibiti vitendo hivyo. Mhandishi Mfugale alieleza zaidi jkuwa ana imani na wananchi wa Mkoa wa Kigoma, kwamba watatoa ushirikiano kuhakikisha vitendo hivyo vya wizi havitokei.

Katika hatua nyingine, Mhandisi Mfugale alisema kuna maeneo wananchi wanataka wakati wameshalipwa kwa muibu wa sheria, hivyo kusababisha miradi ya barabara kuchelewa kuanza.

Kwa upande wake, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika ufunguzi mradi huo, alisema Benki ya Maendeleo ya Afrika itatoa Sh.trilioni moja, na kuishukuru kwa kuendelea kuiunga mkono Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kazi yake ya kuimarisha barabara za lami.

Ndalichako alisema changamoto zilizopo katika sekta ya barabara ni nyingi zikiwamo zile za uhamishaji wa miundombinu ya maji, hivyo kuomba kuwahakikishia wadau wa barabara serikali kupitia Wizara ya Ujenzi kwa kushirikiana na uongozi wa mkoa wa Kigoma watafanya kila la ziada kuhakikisha changamoto zote zinatatuliwa ndani ya muda mfupi.

## Julius Mtatiro afunguka kuanza majukumu u-DC

**Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKUU mpya wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, Julius Mtatiro, ameomba ushirikiano kwa viongozi wenzake katika kuiongoza wilaya hiyo ili kufanikisha kutatua changamoto zinazowakabili wananchi.

Alitoa ombi hilo jana baada ya kula kiapo kwa Mkuu wa mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, mjini Songea.

Mtatiro alisema nafasi aliyopewa ni kubwa, hivyo inahitajika uongozi wa ushirikishwaji ili kufanikisha kutatua changamoto zinazowakabili wanachi.

Mtatiro alimshukuru Rais John Magufuli kwa kumteua kushika nafasi hiyo ambayo ilikuwa inashikiliwa na Juma Homera, ambaye aliteuliwa hivi karibuni kuwa Mkuu wa Mkoa wa Katavi.

"Namshukuru Rais John Magufuli kwa kuniona kuwa ninafaa kumsaidia katika kazi ya ukuu wa wilaya ...na mimi namuahidi kuwa nitafanya kazi kwa nguvu zangu zote ili mwisho wa siku Rais aone kuwa hakukosea kuniteua," alisema Mtatiro ambaye akiwahi kuwa mmoja wa viongozi waandamizi wa Chama cha Wananchi (CUF) kabla ya kujiondoa.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, wakati akiitisha zoezi hilo la kuapisha alimtaka mkuu huyo mpya wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, kwenda kufanya kazi za Wananchi kama Rais alivyomtuma. "Kwa upande wake RC Mndeme alimweleza Mtatiro kuwa: "Katika uteuzi watu wengi wanaweza kukupongeza na wengine wakajenga chuki na wewe bila sababu za msingi, hivyo kikubwa ni kuwatumikia wananchi kwa kufuata miongozo inayotakiwa ikiwamo kufuata maadili."




Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam akikokota mkokoteni uliosheheni mabomba ya plastiki, katika Barabara ya Nyerere, eneo la Kamata, jana, hivyo kumfanya ashindwe kuona nyuma, hali ambayo ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JOHN BADI**

# Sababu kesi ya mke wa Bilionea Msuya kukwama

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam, imeshindwa kuanza kusikiliza kesi inayomkabili mke wa marehemu bilionea Erasto Msuya, Miriam Mrita, na mwenzake dhidi ya mauaji ya dada wa bilionea huyo, Aneth Msuya, baada ya mashahidi na wazee wa baraza kushindwa kufika mahakamani.

Aidha, upande wa Jamhuri ulidai kuwa mashahidi wameshindwa kufika mahakamani kwa sababu hawajapelekewa wito wa mahakama.

Madai hayo yalitolewa jana na upande wa Jamhuri katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Jaji Sekela Moshi aliyepangiwa kusikiliza kesi hiyo.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Mkunde Mshanga akisaidiana na Wakili wa Serikali, Kandid Nasua.

Mshanga alidai kesi hiyo ilipangwa kuanza kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri, lakini kwa bahati mbaya mashahidi hawajatumiwa hati ya wito wa mahakama.

"Mtukufu Jaji, kesi imekuja kusikilizwa, lakini kwa mujibu wa kifungu cha 265 cha Mwenendo wa Sheria ya Makosa ya Jinai (CPA) sura ya 20, kinaelekeza uwapo wa wazee wa baraza wakati wa usikilizwaji wa kesi za mauaji, tunaomba kuahirisha na mashahidi watumiwe hati ya wito," alidai Mshanga na kuongeza: Pia, tunaomba maelekezo yatakayoipendeza mahakama."

Jaji Moshi alisema pamoja na kukosekana wazee na mashahidi kesi hii isingeweza kuendelea kwa sababu ilipangwa kusikilizwa siku mbili na ina mashahidi 45 wa Jamhuri.

"Kesi hii ilipangwa kusikilizwa leo (jana) na Jumatatu ijayo na ina mashahidi wa Jamhuri 45, ambao wote lazima wasikilizwe kwa wakati mmoja, mahakama yangu imeamua kwamba inahitaji muda zaidi, tutaiahirisha ili tuipangie muda wa kutosha."

Upande wa utetezi ukiongozwa na jopo la mawakili watatu, Peter Kibatala, Nehemiah Nkoko na Omary Msemo, ulidai kuwa hauna pingamizi na madai ya Jamhuri.

Jaji alisema washtakiwa warudishwe mahabusu mpaka Naibu Msajili atakapopanga tarehe pande zote mbili zitajulishwa washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu.

Mbali ya Miriam, mshtakiwa mwingine ni mfanyabiashara, Revocatus Muyela.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa wanadaiwa kuwa Mei 25,2016 walimuua kwa makusudi dada wa marehemu bilionea Erasto Msuya, Aneth Msuya.

# WB yaiwezesha Tanzania tathmini baada ya maafa

**Na Mwandishi Wetu**

Benki ya Dunia, kwa kushirikiana na serikali ya Tanzania kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Idara ya Menejimenti ya Maafa, imeendesha mafunzo juu ya namna ya kufanya tathmini ya mahitaji baada ya maafa kutokea na namna ya kuandaa mipango wa kurejesha hali baada ya maafa kutokea. Walengwa walikuwa wataalamu wa menejimenti ya maafa kutoka wizara, mikoa, taasisi na Idara za serikali pamoja na mashirika yasiyo kuwa ya kiserikali. Akizungumza wakati wa kufunga mafunzo hayo, jijini Arusha jana, Mkurugenzi wa Idara ya Menejimenti ya Maafa, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kanali Jimmy Matamwe, alifafanua kuwa lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha kuna wataalam wa kutosha nchini wa kufanya tathmini za maafa kitaalamu zenye kujikita katika athari za maafa katika nyanja za kijamii, kiuchumi na maendeleo.

"Mafunzo haya yatatusaidia kutuongoza serikali na wadau wa menejimenti ya maafa kuwa na mfumo wa pamoja utakaowezesha kuwa na mtazamo wa pamoja katika kuendesha shughuli ya tathmini husan kwa athari za kiuchumi kwa ngazi ya mtu binafsi, taifa na kimataifa, uharibifu wa miundombinu na hapo tutaweza kuwa na mpango wa pamoja wa kurejesha hali, " amesema Matamwe.

Matamwe ameendelea kufafanua kuwa kutokana na wataalamu hawa kujengewa uwezo wa kuandaa mpango wa kurejesha hali, utaalamu huo utaisaidia Tanzania kuwa na takwimu za urejeshaji hali na kupata uwezo wa kurejesha hali itakayo saidia nchi kuwa inarejesha hali kwa wakati.

Akizungumza kwa niaba ya Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia nchini, Mtaalamu wa Mawasiliano Benki hiyo, Edward Anderson, alieleza kuwa Benki hiyo imeamua kuendesha mafunzo hayo ili Tanzania kuwa na wataalamu wenye uwezo wa kurejesha hali kwa wakati baada ya maafa kutokea. "Tangu mwaka 2016 nilipofika hapa nchini nimeshuhudia athari za maafa yakitokea ikiwamo tetemeko la ardhi mkoani Kagera, na mafuriko katika Jiji la Dar es Salaam mwaka 2016, hivyo maafa yanahitaji mfumo sahihi na mpango bora katika kurejesha hali, na ninafurahi kuona Benki ya Dunia tupo tayari katika kutekeleza hayo," alisema Edward.

# MOI kupeleka kusini matibabu kibingwa

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI) inatarajia kutoa huduma za kibingwa za matibabu na upasuaji wa mifupa katika Hospitali ya Nyangao mkoani Lindi kuanzia mwezi ujao.

Imeeleza kuwa uamuzi huo umelenga kupunguzia wananchi wa mikoa ya Lindi na Mtwara changamoto ya kusafiri hadi Dar es Salaam kufuata huduma inazozitoa.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, akizungumza kuhusu ushirikiano huo jana, alisema taasisi hiyo imekubali kuanzisha ushirikiano na hospitali hiyo ili kuwasogezea huduma za matibabu wananchi wa kanda ya kusini kwa kuwa wamekuwa wakisafiri umbali mrefu kufuata huduma hizo.

"Lengo la Serikali ni kuhakikisha huduma zetu zinawafikia wananchi katika ngazi zote za mikoa na wilaya, hivyo wananchi wa ukanda huu wa kusini wataanza kupata huduma za mifupa na madaktari bingwa wetu watakuwa wanakuja hapa wanatoa huduma kwa wananchi," Dk. Boniface alisema.

Daktari Bingwa wa Hospitali ya Nyangao, Dk. Richard Jankiewics, alisema wamekuwa wakikabiliwa na changamoto kubwa ya uhaba wa madaktari bingwa wa mifupa katika ukanda huo wa kusini hivyo kulazimika kutoa rufaa kwa wagonjwa kwenda MOI kufuata huduma hizo.

"Tunaishukuru MOI kwa kukubali ombi letu la kuanzisha ushirikiano ili walete wataalamu kutibu hapa, ni ukweli usiopingika kwamba ukanda huu wa kusini kuna uhaba mkubwa wa madaktari bingwa wa mifupa, hivyo hatua hii italeta mageuzi makubwa kwenye huduma na naamini wananchi wengi watanufaika," alisifu.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Ligi Kuu Tanzania Bara yahitaji udhamini makini

MSIMU mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2019/20 ambao utashirikisha timu kutoka mikoa mbalimbali nchini, unatarajiwa kufanyika kuanzia Agosti 23 mwaka huu na kumalizika Mei mwakani.

Ligi hiyo inayotoa wawakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, inatarajiwa kushirikisha klabu 20 ambazo ni pamoja na mabingwa Simba, Yanga, Azam FC, KMKC FC, Ruvu Shooting, JKT Tanzania, Mtibwa Sugar, Lipuli FC, Ndanda FC, Kagera Sugar, Mbao FC na Alliance FC.

Timu nyingine ni Mwadui FC, Mbeya City, Tanzania Prisons, Biashara United, Coastal Unional, na mbili zilizopanda daraja ambazo ni Namungo na Polisi Tanzania.

Ligi hiyo inayochezwa kwa mfumo wa nyumbani na ugenini, inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinatokana na klabu hiyo kukosa fedha.

Tofauti na timu za mataifa mengine, hapa nchini ni timu chache ambazo zinaendesha shughuli zake kwa kutegemea udhamini binafsi wa klabu husika au taasisi ambayo inaimiliki timu hiyo.

Timu ambayo inaweza kujiendesha bila ya kuumiza kichwa ni Azam FC, huku watani wa jadi, Simba na Yanga wao wanaweza kujiendesha kwa ahadi, kwa sababu wanakopesheka, kutokana na kuwa na mtaji wa mashabiki.

Timu nyingine zilizobakia, ukizitoa zile zilizoko chini ya taasisi za kijeshi, zinajiendesha katika mazingira magumu na yasiyoridhisha au yasiyofanana na ukubwa wa ligi husika.

Msimu uliopita tumeshuhudia kuona klabu ya Coastal Union ikifika jijini Dar es Salaam, saa chache kabla ya kuanza kwa mechi yake dhidi ya Simba, mchezo ambao ulimalizika kwa wenyeji hao wa Tanga kupokea kichapo cha mabao 8-1.

Uongozi wa klabu hiyo haukuwa tayari kuweka wazi kilichosababisha wakachelewa kufika jijini, lakini ni wazi kwamba suala la maandalizi ya safari ya kuileta timu yao lilikuwa halijakamilika na yote haya yalisababishwa na ligi kukosa mdhamini.

Nipashe linaamini kwamba, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limeziona changamoto zote ambazo wanachama wake walizipata katika msimu ulipita, hivyo ni wakati muafaka wa kuhakikisha mdhamini atakayepatikana awe ni mwenye kupunguza makali hayo ya uendeshaji wa timu.

TFF ihakikishe mdhamini anayepatikana anaweza kutoa fedha ambazo zitasaidia kulipia gharama za usafiri angalau asilimia 70 ya mechi zote za msimu mzima, huku kiasi kilichobakia kikaachwa kwa mashabiki kujitokeza kushangilia timu zao.


Hili la mashabiki kujitokeza uwanjani, linawezekana kama ilivyowezekana kwa Simba iliyorejea nchini ikiwa imefungwa mabao 10 kwenye mechi za ugenini, lakini mashabiki wake waliaminishwa kwamba kwenye Uwanja wa Taifa hakuna mgeni atakayetoka salama, na hiyo kampeni yao ilifanikiwa na ingependeza kuona mashabiki wa mikoani wanajitokeza kushangilia klabu zao.

Kama msimu uliopita ilikubali kujifunga "mkanda" kwa kuendesha ligi isiyokuwa na mdhamini, ni vema ikahakikisha pia msimu ujao inakuwa na mdhamini ambaye ataonekana kuwa na faida kwa timu na asiwe ni bora mdhamini.

Kikosi cha Wachezaji wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), kinategemea kutoa wachezaji wengi kutoka katika Ligi Kuu Tanzania Bara, hivyo kufanya vizuri wa ligi hii, ndiyo maandalizi ya kupata kikosi imara cha Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

## Mgema akisifiwa, tembo hulitia maji

**'MGEMA'** ni mtu anayefanya kazi ya kukinga tembo (kileo kinachogemwa kutoka kwenye mnazi, mvumo, mchikichi, mkoche) au kuchanja magome ili kupata utomvu. Kwa ufupi ni mtu anayetengeneza tembo (pombe) la mnazi.

Wahenga walisema: "Mgema akisifiwa, tembo hulitia maji." Maana yake mgema apewapo sifa kutokana na tembo lake, badala ya kulitengeneza tembo zuri hulitia maji na matokeo yake ni kuliharibu. Ni tamaa ya kupata hela zaidi.

Hebu soma sifa za magazeti yetu ya michezo kwa timu zetu za kandanda, hasa Simba na Yanga: "Tuacheni, tutawaziba midomo" ni kichwa cha habari kwenye ukurasa wa kwanza wa gazeti husika. Simba watamba: "Tukirudi mtakoma." "Yanga moto ... nyuma chuma, mbele wembe." "Jeshi laYanga tetemeko CAF!" Tetemeko la nini? Ajuaye ni mwandishi mwenyewe!

Hii ni mifano michache ya vichwa vya habari kwenye magazeti ya michezo nchini kuzishabikia mno Simba na Yanga kumbe zinawaharibu wachezaji kwa kuwapa sifa wasizostahiki! Ni yale yale ya "mgema akisifiwa, tembo hulitia maji."

Kadhalika "Simba ambaye ni mngwizi halii." 'Mgwizi' ni mnyama anayewakamata wengine. Maana yake Simba aliye stadi kuwagwia (kitendo cha kukamata; shika) wanyama wengine hajitangazi au kulia.

Methali hii hutumiwa kumpigia mfano mtu anayejisifu kwa uwezo fulani. Badala ya kujisifu ni heri akafanya jambo likaonekana. Pia huweza kutumiwa kumdhihaki mtu anayejisifu kuwa na ujuzi fulani.

Ni dhahiri kuwa waandishi wa magazeti ya michezo huzipamba sana Simba na Yanga ili yanunuliwe kwa sababu ndizo timu zenye wapenzi na mashabiki wengi zaidi nchini. Ukichunguza sana utagundua kuwa baadhi ya waandishi hao huandika kwa kuwasifu kupita kiasi wachezaji wa timu wazipendazo kumbe wanawaharibu! Naam, "mgema akisifiwa, tembo hulitia maji."

"Marcelo acha kabisa ni fundi wa kupiga pasi, krosi za hatari, kwa kujichimbia ndio usiseme." "Mavitu ya AFCON yaanza Yanga." Simba huko Sauzi ni moto yapiga tizi la kimataifa uso kwa uso na Orlando Pirates." "Kombinesheni Yanga ni kanyaga twende. Balama, Tshishimbi, Makame ni habari nyingine."

Ni baadhi ya vichwa vya habari za magazeti ya michezo hivi karibuni. Kila kichwa kina sifa zisizowezekana wala kutokuwepo kwa vilabu na wachezaji wao almuradi (bora tu) magazeti yanununliwa! Huu ni sawa na wizi wa kimazingaombwe au kamari ya 'pata potea, mzungu kalala hapa ... kalala pale ...'

Waandishi wanapaswa kutambua kuwa katika mchezo wowote kuna tofauti ya mazoezi na mashindano. Kuna wakati wachezaji hawajitumi sana mazoezini kama wanavyocheza mechi za ushindani na timu zingine. Baadhi yao huogopa kuumia; hivyo hufanya mazoezi kwa tahadhari kubwa ili wasishindwe kucheza mechi halisi.

Ushauri wangu kwa waandishi wa habari za michezo ni kutowasifu sana baadhi ya wachezaji wanapokuwa mazoezini kwani kuna hatari ya kujiona bora kuliko wenzao. Kiburi hicho chaweza kuwafanya wacheze kwa mbwembwe na dharau kwenye mechi za mashindano, kumbe wanaharibu na kufanya wazomewe na watazamaji!

Zamani, kandanda ilichezwa kustarehesha watazamaji na kuwa mazoezi maalumu kwa wachezaji ambao hawakuwa wakilipwa chochote. Siku hizi kandanda ni ajira, yaani kazi inayofanywa kwa malipo. Wachezaji wanaolichezea 'gozi la ng'ombe nyama kala nani' na kufuata taratibu zote za mchezo huo yakiwemo maelekezo ya walimu, sasa ni matajiri wanaolipwa mishahara mikubwa kuliko hata wakuu wa nchi zao!

Wanaosumbuliwa na ujana wamenunua magari mengi yanayofikia matano au zaidi ili kuwastarehesha na 'washikaji'! Wengine wana boti (chombo kidogo cha moto cha kusafiria baharini; mataboti) za starehe na baadhi wamenunua ndege (eropleni). Wenye kuona mbele wana miradi mikubwa katika nchi zao kama ujenzi wa hospitali, vituo vya kufundishia vijana mchezo wa kandanda ili kuzinufaisha nchi zao baadaye n.k.

Mbwana Samatta ametumia hela anazopata Ulaya kujenga Msikiti utakaotumiwa na umati wa Mtume Muhamad (SAW). Maana yake nini? Anamshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo aliompa kucheza kandanda. Ili kumrejeshea shukrani, amejenga jengo la ibada kwa Waislamu wenzie waishio jijini Dar es Salaam.

Fikiri ni thawabu gani anazopata kwa Mwenyezi Mungu kwa kuwakumbuka Waislamu wenzake. Hapana shaka swala (ibada katika dini ya Kiislamu iliyo ya lazima kwa Muislamu kama mojawapo ya nguzo tano za Uislamu) zinazofanyika hapo zinazidi kumsitawisha Samatta kiimani katika maisha yake duniani.

Samatta ameamua kujitengenezea njia nzuri ya maisha ya baadaye baada ya kufufuliwa. Mungu akujaalie (kitendo cha Mwenyezi Mungu kusababisha jambo liwezekane) Inshallah!

**marobarnabas@yahoo.com 0784 334 096**

# Serikali yataka nguvu ya wadau ukatili watoto

**Na Elizabeth Zaya**

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imesema bado kunahitajika kuunganisha nguvu za pamoja na wadau mbalimbali katika kukemea na kudhibiti vitendo vya ukatili kwa watoto nchini.

Kaimu Mkurugenzi wa Wizara hiyo (Idara ya Maendeleo ya Watoto, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii), Mwajuma Mawiza, alisema vitendo vya ukatili kwa watoto haviwezi kumalizwa na mtu mmoja bali vinahitaji kupambana kwa pamoja na wadau wote.

Akizungumza katika hafla ya Shirika la Kimataifa linalohudumia watoto la Save the Chidren ya kusherehekea miaka 100 ya utoaji wa huduma, Mawiza alisema wao kama wizara husika, tayari wameweka mikakati mbalimbali inayowashirikisha wadau mbalimbali wa sekta za umma na binafsi ikiwamo Shirika linalishughulika na kazi ya kusaidia watoto la Save the Chidren kuhakikisha wanakomesha vitendo vya ukatili dhidi ya watoto hao.

"Sisi kama serikali tumeandaa mpango wa pamoja, kati yetu na wadau mbalimbali, tunao mpango wa kutokomeza ukatili kwa wanawake na watoto (Mtakua) unaotarajiwa kuisha mwaka 2021 na katika maeneo nane ambayo mengine yanatekelezwa na Save the Chidren na wadau wengine," alisema.

"Lakini nataka niwaombe Watanzania kwamba kutokomeza ukatili kwa watoto ni jambo ambalo linahitaji kufanywa na kila mmoja, siyo mashirika na serikali peke yake, bali hata mwananchi mmoja mmoja, kila mtu akitekeleza kwa juhudi tutafanikiwa."

Kwa upande wake Ofisa kutoka Shirika la Save the Chidren, Touma Nkwabi, alisema wamejiwekea mikakati katika maeneo makuu nane ikiwamo kuhakikisha mtoto analindwa, anapata fursa ya kujifunza, anaishi salama, anapata lishe bora, elimu, hanyanyaswi, analindwa dhidi ya umasikini, na anapatiwa haki zote za msingi.

Nkwabi alisema katika uzoefu wa miaka mingi wa kuhudumia watoto Tanzania, wamebaini kwamba changamoto nyingi zinazowakumba watoto hao ni pamoja unyanyasaji na kupata mimba za utotoni.

Changamoto nyingine alisema ni uwapo wa vifo vya watoto wachanga, utapiamlo na kutokupatiwa haki zao za msingi ipasavyo.

# TMA kutoa tahadhari hali ya hewa Ziwa Victoria

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), kwa kushirikiana na wadau imeandaa mpango maalumu wenye lengo la kuongeza ufanisi wa utoaji wa tahadhari za hali mbaya ya hewa kwa watumiaji wa Ziwa Victoria.

Mpango huo ulibainishwa wakati wa uzinduzi rasmi wa mradi wa 'HIGH Impact Weather lAke System (HIGHWAY)', uliofanywa na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA Dk. Ladislaus Chang'a, jijini Dar es Salaam, jana.

Akizungumza kwenye uzinduzi huo, Dk. Chan'ga, alisema TMA imedhamiria kusambaza kwa wakati taarifa za hali ya hewa.

"Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imedhamiria kuongeza ufanisi wa uandaaji na usambazaji kwa wakati wa taarifa za hali ya hewa hususani taarifa za hali mbaya ya hewa kwa watumiaji wa Ziwa Viktoria," alisema Dk. Chang'a. "Wadau wa mradi huu wakiwamo wataalam kutoka TMA watakaa pamoja na kufanyia maboresho taarifa zinazotolewa na Mamlaka na hivyo kufanikisha utoaji wa huduma bora zaidi," alisema. Awali, wakati wa ufunguzi huo, Rita Roberts, ambaye ni mtaalam wa mradi kutoka 'National Centre for Atmosphere Research (NCRA)' alifafanua kuwa mradi huo utasaidia Kanda ya Afrika Mashariki.

Alisema kupitia taasisi zake za hali ya hewa mradi utafanikisha utoaji endelevu wa tahadhari za hali mbaya ya hewa kwa wakati pamoja na kuongeza kiwango cha usahihi na uhakika kwa taarifa za hali ya hewa na hivyo kupunguza athari za vifo na upotevu wa mali.

Mradi huo unahusisha Taasisi za Hali ya Hewa za Tanzania, Kenya, Uganda na Rwanda kwa kushirikiana na Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) na 'National Centre for Atmosphere Research (NCRA)' kutoka Marekani, Taasis ya Hali ya Hewa ya Uingereza (UKMet Office) kwa ufadhili wa 'Department for International Development (DFID)' ya Uingereza.



Meneja wa Kanda ya Mashariki wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Venance Mashiba (wa nne kushoto) na Mkurugenzi wa Wateja Binafsi wa Benki ya NBC, Gaudence Shawa (wa pili kulia), wakikata utepe kuzindua rasmi tawi jipya la Benki ya NBC Tegeta nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waliofanya vizuri Biashara kidato 6 wazawadiwa vyeti

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Wahasibu (TAA), kimetoa vyeti kwa wanafunzi 20 waliofanya vizuri masomo ya Biashara katika matokeo ya kidato cha sita mwaka huu, lengo likiwa ni kuwahamasisha kusomea taaluma hiyo.

Vile vile, wametoa vyeti hivyo ikiwa ni kuunga mkono juhudi za waasisi wa TAA akiwamo marehemu Dk. Reginald Mengi, ambao waliianzisha miaka 36 iliyopita, kwa lengo la kukuza na kuendeleza taaluma hiyo nchini.

Mwenyekiti wa TAA, Peter Mwambuja, aliyaeleza hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano wa kutangaza viongozi wa chama hicho na kutoa vyeti kwa wanafunzi 10 wa kike na 10 wa kiume waliofanya vizuri katika masomo ya biashara.

"Leo tumewaita kuwatangazia uongozi mpya ambao umechaguliwa katika mkutano mkuu ulifanyika Juni, mwaka huu. Lakini pia tunayo furaha kuwapatia zawadi wanafunzi 10 bora 20 wa kike na kiume waliofaulu vizuri masomo ya biashara ambao wa kwanza hadi watatu tumewapa vyeti na fedha na kuanzia wa nne mpaka wa saba tumewapatia vyeti," alisema Mwambuja.

Pia, alisema katika kipindi cha miaka miwili ya kuongoza chama hicho, wanatarajia kukifanya chama cha wahasibu nchini kuwa mlezi halisi wa taaluma hiyo.

Alisema wamejipanga kutoa mahitaji ya msingi kwa maendeleo ya taaluma, serikali na umma kwa ujumla kuhusu masuala ya fedha, uhasibu na ukaguzi na kuwa mnadhimu wa taaluma ya uhasibu na ukaguzi kwa kusaidiana na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA).

Naye Gift Mwakikusi, mwanafunzi aliyeshika nafasi ya nne kitaifa katika masomo ya Biashara, alisema kupewa kwa vyeti hivyo kunatia moyo kuwa jamii na wanataaluma wanatambua juhudi zao.

"Tunaahidi kuendelea kufanya vizuri na kuwa mfano wa kuigwa katika taifa letu lakini pia kuja kuwa watumishi bora katika taaluma tunazoenda kusomea," alisema.

Kwa upande wake Doreen Lipamba, aliyeshika nafasi ya tatu kitaifa katika masomo ya Biashara, aliwashauri wanafunzi wengine wajitume kwa bidii kwa sababu jamii inatambua mchango wao.

Wanafunzi walioshika nafasi 10 bora katika masomo ya biashara katika matokeo yaliyotangazwa wiki iliyopita na Baraza la Mitihani (Necta) ni Noreen Lyimo (Baobab Pwani), Aston Stevin Ngaeje (Kibaha Pwani) na Doreen Lipamba (Benjamin William Mkapa).

Wengine ni Gift Mwakikusi, (Tusiime Dar es Salaam), Emmanuel P. Chila (Alpha Dar) Mery Samwel, Glory Kandonga (Weruweru Kilimanjaro), Merciana Msechu (Mpanda Girls Katavi), Getruda Didoris Ndongo (ST. Christina Girls Tanga) na Athumani Magadura Willium (Umbwe Kilimanjaro).

# Wito wa kutunza vyanzo vya maji

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA wametakiwa kutunza mazingira, vyanzo vya maji na kutumia maji kwa ufanisi ili kuhakikisha huduma za maji zinaendelea kuwapo na kuwanufaisha Watanzania nchini.

Katibu Tawala wa Manispaa ya Kinondoni, Stella Msofe, alitoa rai hiyo jana jijini Dar es salaam wakati akifungua mashindano ya upigaji picha yanayofahamika kwa jina la 'Safal Eye in the Wild'.

Mashindano hayo yana malengo ya kuhamasisha na utumiaji endelevu wa maji na mazingira kwa kutumia lugha ya picha.

"Ili kufurahia ya maji popote ni lazima wananchi kuthamini hata tone moja la maji, tuthamini mazingira na vyanzo vyetu vya maji kwani maji ni uhai pia, " alisema Msofe.

Alisema mfano, kuna viwanda vingi vinatiririsha maji machafu kwa makazi ya wananchi au hata kwa vyanzo vya maji ambavyo yanatumiwa na wananchi jambo ambalo si sahihi na ni uchafuzi wa mazingira pia.

Aliisifu kampuni ya ALAF kwa kufanya mzunguko wake wa majitaka kuishia katika viwanda vyao na kutumika tena jambo ambalo hawachafui mazingira na hata kuwakwaza watu, wala kuchafua vyanzo vya maji pia.

Naye Meneja Masoko wa ALAF, Isamba Kasaka, alisema maji ya kiwandani kwao hapo wameyaongeza thamani na kutumia katika mashamba.

Hata hivyo alisema nidhamu ya matumizi ya maji huanzia nyumbani mtu anapoishi kuanzia anapopiga mswaki mpaka kuoga na matumizi mengine.

"Hata unapokuwa nyumbani unapiga mswaki ukute unafungulia maji kibao yanamwagika chini badala ya kuchota kidogo kwenye chombo na kuyatumia hayo hayo lakini hapana mpaka umwage pasipo kufahamu kuna watu hayo maji yanathamani kwao,"

Kasaka alitangaza tuzo za mshindi atakayepatikana katika mashindano yao kuwa ni pamoja kujinyakulia kitita cha Sh.milioni saba kwa nafasi ya mpigapicha bora wa mwaka kipengele cha dhahabu, kwanza nafasi ya pili kipengele cha silva milioni 4.7 wa tatu kipengeke cha shaba milioni 2.3.

Pia kipengele cha mpiga picha bora wa mwaka kwa picha itakayopendwa zaidi na wananchi zawadi ni milioni 1.7.

Naye Mwanasheria wa Uhifadhi Mazingira, Musa Mnasizu, aliwataka wananchi wanapoona uchafuzi wa mazingira ,uharibifu wa maji ovyo kutoa taarifa kwa mamlaka mbalimbali ili sheria ifuate mkondo wake.

# DC atembelea eneo alikouawa mwanamke kikatili Dar, anena

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Wilaya ya Kigamboni, Sarah Msafiri, amewataka wananchi wa wilaya hiyo kuwa tayari kuripoti matukio ya vitendo vya ukatili wa kijinsia yanayofanywa ndani ya jamii ili kupunguza matukio hayo yanayozidi kushika kasi nchini.

Sarah alitoa wito huo jana, alipotembelea mtaa wa Kizani kata ya Somangila, lilipotokea tukio la Khamis Luwongo (Meshack), anayetuhumiwa kumuua mke wake, Naomi Marijani (36), kisha mwili wake kuuchoma moto na kwenda kuzika majivu.

Alionya kuwapo kwa vitendo vya ukatili uliopitiliza na kuahidi kuwa Serikali itachukua hatua stahiki kwa mhusika baada ya uchunguzi kukamilika.

Alikemea pia matukio hayo kuhusishwa na watu kudaiwa kutekwa na watu wasiojulikana na kuisingizia Serikali na kusema yanachafua taswira ya taifa.

"Nawaomba na wananchi muwe na utamaduni wa kujuliana hali, kujitokeza kwa majirani pale mnaposikia kelele au ishara zinazotilia shaka ili kuepuka vitendo kama hivi," alisema.

Mapema wiki hii, taarifa zilianza kusambaa kwenye mitandao ya kijamii na vyombo vya habari kuhusu kutokea kwa tukio hilo.

Inadaiwa mwanamke huyo alitoweka katika mazingira ya kutatanisha na picha yake kusambazwa katika mitandao ya kijamii ya kutoa taarifa za kutoweka kwake.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Kigamboni, Thobias Walelo, mtuhumiwa huyo anayeshikiliwa na polisi, alikiri kumuua mkewe kisha kumchoma kwa mkaa wa magunia mawili na kumzika shambani kwake.

Alidai mara baada ya mauaji hayo aliuchukua mwili wa mkewe na kuuweka kwenye shimo alilochimba kwenye banda lake la kufugia kuku.

Alidai baada ya kuuweka shimoni, aliweka mkaa magunia mawili na mafuta ya taa kisha akawasha moto ulioteketeza mwili wote hadi kubaki majivu kisha alichukua majivu hayo akaweka kwenye mfuko na kubeba kwa kutumia gari lake lenye namba T206CEJ, Subaru Forester yenye rangi nyeusi na kuupeleka shambani kwake kijiji cha Mlogolo, mkoani Pwani.




# Sababu 2 Lissu kumshitaki Spika Ndugai mahakamani

INATOKA UK. 3

suala hili. Ukiwa maelfu ya kilometa nje ya nchi, halafu unataka mambo yaende sawa Tanzania, unahitaji utulivu na umakini. vinginevyo utafanya makosa yanayotokana na upungufu wa umakini halafu utaonekana siyo mtu makini. Natumaini maelezo haya yatakuwa yamewasaidia kupunguza hofu na kelele," alisema.

"Wanachokiita uchaguzi kimefanyika. Kazi yao imekwisha. Ratiba ya Mahakama inaanza muda wowote kuanzia Juni 29 hadi Desemba 28, mwaka huu. Maana yake ni kwamba ninaweza kufungua kesi katika siku yoyote ndani ya hicho kipindi cha miezi sita.

"Hadi sasa, hazijafika wiki tatu tangu uamuzi wa Spika Ndugai. Bado nina miezi mitano na wiki moja ya kufungua kesi. Kwa hiyo, wanaolialia kwamba nimeachia ngazi, wajue sijachelewa hata kidogo," Lissu alitamba.

Alibainisha kuwa mwenye haki ya kufungua kesi hiyo ni yeye au mwakilishi wake ambaye ampatia mamlaka ya maandishi ya kushtaki kwa niaba (Power of attorney).

"Power of attorney inatakiwa kutiwa saini na mimi mwenyewe mbele ya kamishna wa viapo anayetambuliwa na sheria za Tanzania. Kimsingi, wakili anayefanya kazi Tanzania anatakiwa kuja kunishuhudia sahihi huku niliko," alisema.

Juni 28, Spika Ndugai aliliambia Bunge kuwa amemwandikia Mwenyekiti wa NEC kumjulisha kuwa kiti cha ubunge wa Singida Mashariki kiko wazi kutokana na Lissu kutotoa taarifa kwa Spika kuhusu aliko pamoja na kutojaza fomu za mali na madeni na kuziwasilisha kunakokotakiwa.

Septemba 7, 2017, Lissu alishambuliwa na watu wasiojulikana kwa kupigwa risasi zaidi ya 30 akiwa anajiandaa kushuka kwenye gari lake nyumbani kwake, Area D jijini Dodoma.

Kutokana na shambulio hilo la kinyama lililoharibu mwili wake, Lissu alilazimika kupata matibabu ya kibingwa yaliyoanzia Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma kisha kupelekwa Hospitali ya Nairobi, Kenya na baadaye kuhamishiwa Ubelgiji anakoendelea nayo.

Kabla ya kutangaza kumvua ubunge, Spika Ndugai alisema Bunge linakusudia kuzuia mshahara na posho za Lissu baada ya kuonekana ametoka hospitalini na kufanya ziara katika baadhi ya nchi za Ulaya na Amerika.

# Wanaochungisha watoto mifugo wapewa kibano

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

VIONGOZI wa kimila wa jamii ya wafugaji (malaigwanani) wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, wamepitisha sheria ndogo ya kuwatoza Sh.milioni moja watakaochungisha mifugo watoto wao badala ya kuwasomesha..

Sheria hiyo pia inawabana wazazi ambao wanashiriki katika vitendo vya kuwakeketa watoto wao wa kike.

Wazee hao wa kimila waliyasema hayo wakati wakizungumza jana mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, kwenye sherehe za kimila Kijiji cha Lengast Kata ya Naisinyai. Meibuko Parasoi, alisema wamelenga kuhakikisha mila zilizopitwa na wakati wanaachana nazo na mtu ambaye hatatimiza makubaliano hayo, atatozwa faini hiyo.

Parasoi alisema kwa sababu rasilimali kubwa ya jamii ya wafugaji ni mifugo, wameazimia kuwapa elimu watoto wao ili waendeleze ufugaji wenye tija na kuachana na ukeketaji kwa wasichana.

Chaula aliwapongeza viongozi hao wa kimila kwa kuweka mikakati hiyo ya kupambania vijana wao wasome na kumaliza vitendo vya kikatili vya ukeketaji wasichana.

Chaula alisema wale wanaokeketa wasichana wanapaswa kutambua kuwa suala hilo limepitwa na wakati na hivi sasa linaitwa 'zilipendwa' kwani jamii imestaarabika na kuachana nayo.=

"Watoto wa kike wanasomeshwa, watoto wa kiume wanasomeshwa wote wana haki sawa, pia Malaigwanani mkemee wasichana kupata mimba shuleni na kuolewa wakiwa wadogo," alisema.

Mmoja kati ya wakazi wa kijiji cha Lengast, Elias John, alisema anaunga mkono hatua hiyo kwa sababu bila kuweka faini hiyo vitendo vya ukeketaji na kusomesha watoto wao havitadhibitiwa.

"Wengine wamekuwa wanakeketa watoto wao kwa kisingizio cha kuwa na ugonjwa wa fangasi ukeni maarufu kama 'lawalawa', lakini wanapaswa kuwapeleka hospitali na siyo kuwakeketa," alisema John.

Mkazi wa kijiji cha Lengast, Esupati Mollel, alisema ili kutimiza hayo, Jamii pia ipatiwe elimu na kukubali kubadilika kwa lengo la kwenda na wakati na kuachana na mila kandamizi zisizo na mashiko.

"Sisi wanawake tunaunga mkono suala hilo japokuwa tunaona kutumia sheria ndogo siyo vizuri tofauti na elimu kutolewa na jamii kuacha wenyewe ukeketaji wa wasichana na kuwapeleka shule vijana badala ya kuchungisha mifugo," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo (kulia) na Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, wakipata maelezo kutoka kwa Mkandarasi wa mradi wa umeme wa Tanzania na Kenya m/s Gopa kutoka International Energy Consultant GmbH ya Ujerumani, kuhusu ramani ya ujenzi wa mradi huo unaopita katika vijiji tisa mkoani humo juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wadau waombwa kusaidia watoto mazingira hatarishi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JUHUDI za lazima zinahitajika kufanyika na wadau mbalimbali za kuwasaidia watoto 54,911 wa Mkoa wa Arusha, wanaoishi kwenye mazingira hatarishi na kulelewa kwenye vituo ili waondokane na changamoto zinazowakabili.

Hayo yalisemwa jana na Afisa ustawi wa jamii Mkoa wa Arusha, Denis Mgiye, wakati akizungumza katika semina ya siku tatu kwa wadau wa masuala ya watoto wakiwamo wachungaji, waandishi wa habari, na maofisa maendeleo ya jamii yaliyoandaliwa na shirika linaloshughulika na masuala ya malezi na ulinzi wa mtoto la SOS Children Villages Tanzania.

Alisema kwa takwimu za hadi Machi mwaka huu, wilaya inayoongoza kwa kuwa na watoto wengi ni halmashauri ya Jiji la Arusha ambayo ina jumla ya watoto 21,687 .

Alisema changamoto kubwa ambazo zimekuwa zikichangia kuwapo kwa idadi kubwa ya watoto waishio mazingira magumu ni kuwapo kwa umaskini uliokithiri ngazi ya jamii, migogoro ya ndoa, ukatili wa kupindukia pamoja na wazazi kutowajibika ipasavyo.

Kutokana na hali hiyo, alitaka elimu zaidi kutolewa kwa jamii katika kutambua madhara yanayotokana na migogoro ya kifamilia ili kuwanusuru watoto hao. "Endapo tutaunganisha nguvu wadau wote tutasaidia watoto hawa kuondokana na changamoto zinazowakabili," alisema.

Mratibu Taifa utetezi wa haki za watoto wa shirika hilo, Mpelly Kalonge, alisema lengo la semina hiyo ni kusaidia watekelezaji wa sera za mtoto na wadau wa maendeleo ya mtoto kujadili changamoto zinazowakabili watoto na kutoka na suluhisho la pamoja.

Mpelly alisema kupitia semina hizo wamekuwa wakiangalia kila mdau ana nafasi gani katika kushughulikia kwa pamoja changamoto zinazowakabili watoto na kuongeza nguvu ili kuhakikisha ukatili unaoendelea dhidi ya watoto unakomeshwa.

Aliongeza changamoto kubwa iliyopo katika jamii ni kutokuwapo kwa ushirikishwaji wa kutosha kwa mtoto katika kutoa maamuzi ndani ya jamii, hali ambayo hupelekea mtoto kutokuwa muwazi katika kuelezea changamoto anazokabiliana nazo hususan katika masuala ya ukatili wa kijinsia.

Mmoja wa washiriki katika semina hiyo, Salvatrix Kinabo ambaye ni Mkurugenzi wa kituo cha kulea watoto wadogo wa mchana (daycare) cha St.

James Kingdom alisema kuwa, kumekuwapo na sheria zinazomlinda mtoto ila changamoto iliyopo ni kuwapo kwa usimamizi hafifu katika sheria hizo. Aliwataka wadau mbalimbali pamoja na jamii kwa ujumla kuona suala hilo la kumlinda mtoto ni la kila mmoja, hivyo ni wajibu wa kila mmoja kusimama katika nafasi yake kuhakikisha wanatokomeza changamoto zinazochangia kuwapo kwa watoto wa mitaani na kukomesha suala zima la ukatili wa kijinsia.

# Bashiru aziagiza jumuiya za CCM miradi mikubwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, amezitaka jumuiya za chama hicho kubuni miradi mikubwa ya kilimo na viwanda na kuachana na miradi midogo iliyozoeleka ya kupika maandazi na kupangisha.

Aliyasema hayo wakati akishiriki kuvuna mahindi kwenye shamba la Engusero la Jumuiya ya Wanawake wa chama hicho (UWT) Wilaya ya Kiteto, lililowezeshwa na Mbunge wa Viti maalum wa Mkoa wa Manyara, Martha Umbullah.

Alisema jumuiya za chama hicho zinapaswa kubadilika kwa kubuni miradi endelevu, ambayo itawanufaisha na mwisho wa siku wataondoka katika utegemezi.

"Nashiriki kutekeleza ilani ya CCM kwenye kipengele cha kilimo na viwanda, nina uhakika hili siyo shamba la mtu binafsi, nimeshiriki kuvuna shamba la UWT na Kiteto mmeingia kwenye kumbukumbu yangu," alisema Dk. Bashiru.

Pia, Dk. Bashiru alimpongeza Mbunge wa Jimbo la Simanjiro, James Ole Millya, kuwa ni mahiri, makini na mchapakazi ndiyo sababu wakakubali kumpokea CCM kutoka Chadema , kwani waliwakataa wabunge watatu wa vyama vya upinzani, walioomba kujiunga na CCM baada ya kubaini kuwa hawawezi kukidhi vigezo vya kuwa wabunge wa chama hicho.

Alisema kwenye Mkoa wa Manyara waliwapokea wabunge wawili wa upinzani Ole Millya na Pauline Gekul wa Jimbo la Babati Mjini (Chadema), ambaye alikuwa mwanafunzi wake Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Dk. Bashiru alisema CCM siyo chama cha kuchukua kila mtu, ndiyo sababu waliwakataa hao ambao hata hivyo, hakuwataja majina, akisema kama wangewakubali kuwapokea wote upinzani ungemalizika.

"Tumewakataa wabunge hao watatu waliotaka kuja kwetu kwa kuwa CCM siyo jalala kwa sababu mtu aliyekata tamaa anaweza kujiumiza mwenyewe au kuumiza wenzake," alisema Dk. Bashiru bila kufafanua zaidi kauli hiyo.

Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Manyara, Martha Umbullah, alisema aliipatia UWT Sh. milioni mbili na gharama nyingine za shamba, ili jumuiya hiyo ijiwezeshe kiuchumi.

"Niliona badala ya kuwapatia samaki niwape nyavu wakavue samaki na shamba hilo la mahindi litawasaidia kinamama hawa wa UWT Kiteto katika kujinufaisha kiuchumi," alisema Umbullah.

Kwa upande wake, Millya alisema miradi mingi ya maendeleo iliyofanyika wilayani Simanjiro kupitia Rais John Magufuli, ndiyo sababu yeye kujiuzulu Chadema na kujiunga na CCM.

# Saa 96 za Majaliwa na msako wezi nondo tani tano

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WIZI wa nondo tani tano zilizonunuliwa kwa fedha za umma kwa ajili ya mradi mkubwa wa ujenzi wa stendi ya mabasi ya Ngangamfuni, Manispaa ya Moshi, umemshtua Waziri Mkuu Kasim Majaliwa, na kuagiza waliotekeleza hujuma hiyo wakamatwe katika muda usiozidi saa 96.

Kituo hicho cha kimataifa cha mabasi cha Ngangamfumuni ni mradi mkakati uliopitishwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) na kutengewa Sh. bilioni tisa.

Majaliwa alishangazwa na hali hiyo juzi, baada ya kutembelea na kukagua mradi huo.

Kutokana na wizi huo, Waziri Mkuu alisema Serikali inaweza kusitisha kutoa fedha za ujenzi wa mradi huo endapo matukio ya wizi wa vifaa vya mradi huo utaendelea. Akiwa katika eneo hilo, Waziri Mkuu alimpa siku nne Kamanda wa Polisi mkoa wa Kilimanjaro, Hamisi Issah, kuhakikisha anawakamata walinzi waliokuwa wakilinda mradi huo na endapo atashindwa amkamate mmiliki wa kampuni ya ulinzi iliyopewa zabuni ya ulinzi.

Alisema Serikali imekuwa na utaratibu wa kutenga fedha na kuzipeleka katika halmashauri nchini ili kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ambapo manispaa ya Moshi ilipambana kuona mabasi yanapata stendi baada ya kuona iliyopo haikidhi matakwa na kubuni ujenzi wa stendi ya Sh. bilioni tisa.

Aidha, alisema kituo hicho cha mabasi kitakuwa stendi ya mfano kitakapokamilika kutokana na ramani yake ilivyo.

Majaliwa alisema wakati Serikali ikipambana kuleta fedha ya mradi huo, wananchi wa Moshi wamekuwa wakiiba vifaa vya ujenzi wake na kudai kuwa nondo tani tano zimeshaibiwa.

"Haiwezekani mwananchi akatoka Lindi na kuja kuiba hapa Moshi, ni nyie wenyewe wananchi wa Moshi mmekuwa mkiiba vifaa vya mradi huo na kuanza kuuhumuju mradi huu," alisema Majaliwa.

Alisema ni jambo la fedheha na linalokatisha tamaa kuona Serikali ikileta fedha kwa ajili ya maendeleo, lakini wananchi wanaondoka na mawe pamoja na nondo.

Aliongeza nondo hizo tani tano zilizoibwa hazikutoka hivi hivi bali wahusika walikuja na winji ya kupakilia na kuitega na kuanza kupakia na sio kwamba walichukua mojamoja, na kueleza kuwa serikali imesononeka na wizi huo na kuwa wanapoelekea siko kabisa.

Aidha Waziri Mkuu alimuagiza Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, kuhakikisha anawachukulia hatua wale wote waliobainika kuhusika na wizi huo. "Hawa waliofanya wizi huu malengo yao sio mazuri, wanataka tukwame tusiwe na kituo cha mabasi halafu mabasi yaendelee kusongamana pale kati kati ya mji ...kwanza pale eneo ni dogo na sisi lengo letu mabasi madogo ndio yabaki katikati ya mji," alisema Majaliwa.

Kwa mujibu wa Majaliwa, hali hiyo ya wizi ikiendelea Serikali haitasita kusitisha ujenzi wa mradi huo na fedha hizo kupelekwa sehemu nyingine ambapo watu wanasubiria fedha ili kupeleka maendeleo.

Aliwataka wananchi kila mmoja kuwa mlinzi wa mwenzake na pindi wanapoona mtu anaiba kifaa chochote katika mradi huo kutoa taarifa kwa jeshi la polisi au watoe taarifa kwa kiongozi wa Serikali.



Mbunge wa Simanjiro mkoani Manyara, James Ole Millya, akizungumzia maendeleo yaliyofanyika jimboni kwake, wakati wa ziara ya Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, katika Mji mdogo wa Orkesumet juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Waamua kuachana na mila zinazodhalilisha wanawake

**Na Mary Mosha,** MOSHI

UONGOZI wa kimila wa jamii ya wafugaji umeamua kuachana na mila potofu ambazo zinawadhalilisha wanawake, watoto na kuwaletea madhara lengo likiwa kumkomboa mwanamke na kumpa elimu bora.

Hakikisho hilo lilitolewa na kiongozi wa kimila wa jamii hiyo, Aman Saisa, wakati wa mkutano ulioandaliwa na shirika lisilo la kiserikali linalojishughulisha na masuala ya uwezeshaji wa kiuchumi kwa makundi maalumu yakiwamo ya wanawake na vijana TUSONGE, uliofanyika eneo la Mikocheni, Kata ya Arusha Chini, Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro.

"Niko tayari kushirikiana na Serikali katika kutokomeza mila potofu ndani ya jamii yetu na pia tuko tayari kwenda kuwaambia wanaohusika na shughuli za ukeketaji wa wasichana (Ngariba), waachane na shughuli hizo," alisema Saisa. Mwenyekiti wa kijiji cha Mikocheni, Koroma Kwenase, alisema vitendo vya ukeketeji vimepungua kwa asilimia 90 katika eneo hilo na kwamba hali hiyo imechangia idadi ya wanafunzi kuongezeka mashuleni.

"Wanafunzi waliokeketwa walikuwa wakikaa ndani kwa muda mrefu kiasi cha kukosa masomo kwa muda wote huo, hali iliyofanya idadi ya mahudhurio kushuka," alisema. Aidha, alisema kupitia elimu iliyotolewa, watu wameelimika na ndiyo sababu ya kupungua kwa vitendo hivyo vya kikatili.

Kiroriti Mtero, mmoja wa wazazi, alisema elimu waliyoipata itawasaidia kuepukana na mila potofu. "Sisi kama wazazi wa kiume pindi pale mtoto wangu alikuwa akifanyiwa ukeketaji tulikuwa tunatoa gharama za kumlipa ngariba ambayo alikuwa akija kumkeketa, mara atakapo maliza kazi yake tunamlipa Sh. 20,000 na kwa siku ngariba mmoja alikuwa akikeketa watoto 20," alisema.

Mtero alisema baada ya mtoto kufanyiwa ukeketaji alikuwa akikaa ndani kwa mwezi mmoja kama hajapata madhara na kuwa alikuwa anatunzwa kama mzazi kwa kumpatia mafuta ya ng'ombe, damu na nyama ili kuweza kurudishia damu iliyomwagika wakati akifanyiwa tendo la ukeketaji. Aliendelea kusema kuwa iwapo mtoto atapata tatizo la kutokwa na damu kwa muda mrefu ndipo alikuwa anapelekwa hospitalini baada ya kuwasiliana na madaktari.

"Tunalishukuru sana shirika hili la TUSONGE kwa kuja katika maeneo yetu kutupatia elimu hii kwani imesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza ukeketaji," alisema.

Alisema changamoto iliyopo ni ile ya baadhi ya watu kuendelea kufanya ukeketaji kwa kificho, na wamekuwa wakiwafanyia watoto wachanga wanapozaliwa.

Mmoja wa watoto waliokuwa wametayarishwa kwenda kukeketwa, Elizabert Koromo (13), alisema mzazi wake alikuwa tayari ameandaa ng'ombe na mbuzi kwa ajili ya shughuli ya kukeketwa. Mtoto huyo ambaye ni mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Mikocheni, aliipongeza Tusonge kwa kukemea vitendo hivyo jambo ambalo limewaokolea maisha yao ya kukeketwa.

"Dada zangu wote watano, walishafanyiwa vitendo vya ukeketaji, hivyo walikuwa wakiniambia kuwa siku itakapofika ya kwenda kukeketwa, unapatwa na maumivu makali na unatokwa na damu nyingi," alisema.

Mkurugenzi wa Tusonge, Aginatha Rutazaa, alisema mila potofu, ndoa za utotoni, vipigo kwa wanawake na watoto kutokumilika ardhi, zimekuwa zikichangia kwa kiasi kikubwa kurudisha nyuma shughuli za maendeleo.

# Mghwira ataja dawa migogoro

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, amewataka wananchi wanaoishi katika vijiji vya Mtakuja na Mserikia katika Wilaya ya Moshi kuanza kupunguza idadi ya mifugo kwa kuuza ikiwa ni njia mojawapo ya kukabiliana na migogoro ya kugombea maeneo ya malisho kati ya wafugaji na wakulima.

Alisema kuna haja ya jamii hiyo kuanza kufuga kisasa na kupunguza idadi ya makundi makubwa ya mifugo ambayo yamekuwa yakiharibu mashamba ya wakulima na kusababisha migogoro ya mara kwa mara.

Alitoa agizo hilo juzi, wakati akizungumza na wananchi wa vijiji juu ya njia bora za kumaliza migogoro kati ya makundi hayo mawili.

"Viongozi wa vijiji hivi viwili, nataka muandae mpango mkakati wa kuisaidia jamii ya wafugaji kuwa na shughuli mbadala za kuwaingizia kipato, "alisema na kuongeza:

"Aidha naagiza na ninyi wafugaji fikirieni kupunguza sehemu ya mifugo yenu na kubakisha idadi ndogo ya mifugo kwa sababu ongezeko la watu limesababisha ardhi kuwa finyu na haitoshi kwa malisho na kilimo."


Baada ya kauli hiyo, baadhi ya jamii ya wafugaji katika eneo la

Mserikia akiwamo Lomayani Alaisi, alisema hawana tatizo na agizo hilo kwa kuwa wanafahamu linalenga kuwahimiza kufuga kisasa na kuepukana na migogoro isiyo ya lazima.

"Mimi binafsi sina tatizo na nitatii agizo la serikali la kutaka

kupunguza mifugo na kuanza kufuga mifugo ya kisasa, naijua adha kubwa ninayoipata kipindi cha kiangazi tunapohama na makundi ya mifugo kwa ajili ya kuitafuta malisho katika mikoa ya jirani. Kazi kubwa iko kwa wenzangu kukubaliana na jambo hili ambalo kwao ni gumu," alisema. Lomayani

Diwani wa Mabogini (Chadema), Emmanuel Mzava, akizungumza mbele ya mkuu huyo wa mkoa, alisema wameanza utaratibu wa kutenga maeneo ambayo hayajaendelezwa kwa ajili ya malisho.





Mkurugenzi wa Mipango kutoka Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Bezil Ewala (kushoto), akiwasilisha taarifa ya malengo mkakati na kazi zilizopangwa kutekelezwa na taasisi hiyo, kwa mwaka 2019 – 2020, wakati wa kikao cha Wakurugenzi wa Taasis zilizopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

# Waziri awaita Takukuru hofu ulaji mradi wa maji

**Na Renatha Msungu,**
KONDOA

SERIKALI imesema itashirikiana na Taasisi za Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kufanya uchunguzi kujiridhisha na utekelezaji wa mradi wa maji katika Kijiji cha Masange wilayani Kondoa.

Naibu Waziri wa Maji, Juma Aweso, aliyasema hayo alipozungumza na wananchi wa kijiji hicho katika ziara yake ya kukagua miradi ya maji ukiwamo huo uliogharimu Sh. milioni 433.288.

Alisema atawashirikisha Takukuru kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa mradi huo kutokana na kutoridhishwa na maelezo yaliyotolewa kwake na mkandarasi wa mradi huo.

Mradi huo umetekelezwa chini ya usimamizi wa Kampuni ya Best One.

"Haiwezekani tukauziwa mbuzi kwenye gunia, lazima tukague na kujionea wenyewe baada ya kupewa majibu ya kusuasua. Tutashirikiana na Takukuru ili kubaini ubadhirifu na mkandarasi asilipwe mpaka tujiridhishe na uchunguzi," Aweso alisema.

Awali, akitolea ufafanuzi kuhusu hoja mbalimbali zilizowasilishwa kwake na wananchi wa kijiji hicho kuhusu sekta ya maji, Aweso aliwataka wananchi kuwa na subira, akiwaahidi kuchimbwa visima viwili kijijini huko hivi karibuni.

Alisema taratibu za upatikanaji wa gari la kuchimba visima hivyo zinashughulikiwa.

Mbunge wa Jimbo la Kondoa Vijijini, Dk. Ashatu Kijaji (CCM), alisema yuko tayari kufanya kazi usiku na mchana kutekeleza alichoagizwa na wananchi wa jimbo hilo.

Dk. Ashatu ambaye pia ni Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, alisema adha kubwa kwa wananchi wa Kijiji cha Masange ni ugumu wa upatikanaji wa maji, hivyo kuna haja Serikali kuchukua hatua za haraka kutatua kero hiyo.

Akisoma taarifa ya mradi wa maji wa kijiji hicho mbele ya Aweso, Kaimu Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa) Wilaya ya Kondoa, Falaura Kikusa, alisema mradi huo ulianza Desemba 15, 2014 na ulizinduliwa rasmi Septemba 13, 2016 kupitia mbio za Mwenge wa Uhuru ukigharimu Sh. milioni 433.

Alibainisha kuwa muda wa utekelezaji wa mradi huo kwa mujibu wa mkataba ni miezi minne kuanzia tarehe waliokabidhiwa ambayo ni Desemba 15, 2014 hadi Machi 15, 2015.

Alisema kutokana na changamoto mbalimbali, hususani kuchelewa kwa malipo ya madai ya mkandarasi, mradi uliongezwa muda wa utekelezaji na kutakiwa kukamilika rasmi Juni 7, 2018.

Alisema kijiji hicho kinakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa maji kutokana na ongezeka la wakazi na kukua kwake.

Alibainisha kuwa uwezo wa chanzo cha maji kilichopo ni kutoa lita 119,577.6 kwa siku wakati mahitaji halisi kwa sasa ni zaidi ya lita 141,560 kwa siku.

Kaimu meneja huyo pia alibainisha kuwa mkandarasi wa mradi huo hadi sasa ameshalipwa Sh. milioni 347.421 kati ya Sh. milioni 433.288.

# Ahimiza uwekezaji zaidi bima majanga ya moto

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI imewaomba wadau wa bima kuwekeza zaidi katika huduma ya utoaji kinga za majanga ya moto ili kuwavutia wawekezaji kuwa na uhakika wa biashara wanazowekeza katika maeneo mbalimbali nchini.

Rai hiyo ilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, wakati wa maazimisho ya Siku ya Bima ya Kanda ya Kati.

Dk. Mahenge alisema kuna kila sababu ya kampuni hizo kutoa huduma ya kinga ya majanga ya moto, afya na nyingine ambazo ni muhimu kwa jamii ili kuwavutia wawekezaji kutokana na kwamba watakuwa na uhakika na biashara wanazofanya. Alisema kwa sasa taifa linaelekea katika uchumi wa viwanda na kila mmoja anapaswa kuangalia fursa inayoweza kumpa faida yeye binafsi na taifa kwa ujumla na kuifanyia kazi kiufanisi.

"Naomba kampuni za bima changamkieni fursa za uwekezaji katika huduma ya kinga, lengo ni kuona kila mmoja anatoa huduma za uhakika," Dk. Mahenge alishauri.

Alisema bima ni muhimu kwa sababu ni mpango ambao unaisadia jamii kuepuka kuanguka kiuchumi kutokana na kwamba watakuwa na uhakika wa usalama wao.

Kiongozi huyo wa mkoa pia alisema hakuna sababu ya kubagua watu katika utoaji wa huduma za afya kwa kampuni za bima.

# Vikundi 33 vyapewa mikopo ya mamilioni

**Na Peter Mkwavila,**
CHAMWINO

VIKUNDI 33 wilayani Chamwino vimepata mikopo ya Sh. milioni 105.1 zinazotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri. Kati ya vikundi hivyo, 23 ni vya wanawake, vinane vya vijana na viwili vya walemavu.

Akizungumza katika ziara yake ya kutembelea vikundi hivyo, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ya Chamwino, Sophia Swai, aliwitaka kuelekeza fedha hizo kwenye malengo yaliyokusudiwa ili mikopo hiyo iwe fursa ya kuwainua kiuchumi wananchi.

Ofisa huyo aliwataka waliopata mikopo hiyo kuzalisha bidhaa zenye ubora ili kuwa na soko la uhakika na wahakikishe wanarejesha mikopo kwa wakati.

"Rejesheni mikopo kwa uaminifu na mkope tena, pia muwatafute mabinti waliozaa wakiwa chini ya miaka 18 ili nao wajiunge kwenye vikundi vya vijana ili kupata mikopo na kujiinua kiuchumi," aliagiza.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Ujirani Mwema kilichonufaika na mikopo hiyo, Sarah Chimangha, alisema kina wanachama 29 na wamepata mkopo wa Sh. milioni 2.5 ambao anaamini utawasaidia kuendesha shughuli zao ikiwamo kufungasha chumvi kwenye vifungashio vyenye ubora.

Stella Madelemu, kiongozi wa Kikundi cha Tubebane kilichoko Kijiji cha Mahama, Kata ya Chilonwa, alisema ni mara yao ya kwanza kupata mkopo na watahakikisha wanaboresha kazi zao.

Alisema wamekuwa wakijishughulisha na kilimo cha alizeti na ufugaji na mkopo wa Sh. milioni 1.5 walioupata utasaidia kuboresha kazi zao za kila siku.








Kaimu Afisa Udahili Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Innocent Mgeta (kushoto), akimsajili mwanafunzi anaetarajia kujiunga na chuo hicho, Zulfa Hassan Hussein, katika Maonyesho ya 14 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waikumbusha Serikali Mkataba wa Marrakesh

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Watu Wasioona, kimelitaka Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Wawakilishi kuridhia mkataba wa kimataifa wa Marrakesh, kuwawezesha wanafunzi wenye ulemavu wa kuona na uoni hafifu kufanya vizuri katika mitihani yao.

Mkataba huo unalinda haki za kuwawezesha watu wenye ulemavu hususan wasioona na wale wenye ulemavu wa kusoma maandishi ya kawaida kupata haki na fursa ya kujisomea maandishi yaliyowekwa kwenye mfumo wa maandishi rafiki kwao.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini Zanzibar, mhasibu wa chama hicho, Kombo Mwinjuma Kombo, alisema wanafunzi wengi wanapata shida ya kusoma vitabu shuleni kwa sababu hawaoni na kupelekea kufeli mitihani yao.

Alisema mkataba huo unawezesha watu wasioona kuweza kusoma ambayo ni haki yao ya msingi.

"Iwapo mkataba huu utaridhiwa na wabunge na wawakilishi, matumaini yetu kuwa ufaulu wa wanafunzi wasioona utaongezeka katika mitihani yao ya taifa,"alisema Kombo.

Alieleza kuwa mkataba huo una lengo mahususi la kusaidia na kuwezesha wasioona na wale wenye ulemavu wa kusoma maandishi yasiyorafiki kwao, kuwezeshwa ili wasome na kufaulu kama wengine wenye macho timamu.

Aidha, alieleza kuwa haki na fursa ya watu wasioona ya kupata elimu, kufanya utafiti na kupata habari kwa mifumo na njia nyingine za mawasiliano inakwama kutokana na uwezo mdogo. "Kunahitajika sana kuridhiwa kwa mkataba wa Marrakesh na Serikali ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa una manufaa makubwa kwa walengwa na nchi kwa ujumla... hivyo tunawaomba watoa maamuzi kuharakisha kuridhiwa kwa mkataba huo,"alisema Kombo.

Mratibu wa Jumuiya ya Watu Wasioona Zanzibar, Adil Muhammed, alisema kuwa mkataba huo huwawezesha watu wenye ulemavu hususan wasioona na wale wenye ulemavu wa kusoma maandishi ya kawaida kupata haki na fursa ya kujisomea maandishi yaliyowekwa kwenye mfumo wa maandishi rafiki kwao. Alieleza kuwa mkataba huo unatambua na kuhimiza kuwa mashirika ya serikali na yale yasiyokuwa na kiserikali kuwajibika katika kuwapatia wasioona na wale wenye ulemavu wa kusoma mbadala wa mtindo wa kupata vitabu na machapisho ambao wanaweza kuutumia kupata elimu na upatikanaji wa habari.

# Zanzibar yaridhishwa na ufaulu mwaka huu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imeeleza kuridhishwa na kiwango cha ufaulu wa wanafunzi wa kidatu cha sita, uliofikiwa katika mtihani wa taifa mwaka huu, ambacho kimeongezeka na kufikia asilimia 88.96.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Mohamed Said, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari, kutoa tathmini ya matokeo ya mtihani wa kidatu cha sita uliofanywa mwezi wa Mei mwaka huu na matokeo yake kutolewa hivi karibuni na Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA).

Naibu waziri huyo alisema wanafunzi 1,837 wa shule za Zanzibar walifanya mtihani huo kati ya 2,090 wamefaulu kwa kupata daraja la kwanza hadi la tatu. Aliyataja mafanikio hayo yanatokana na Wizara ya Elimu kuongeza mikakati kwa wanafunzi unaotokana na upatikanaji wa vifaa vya elimu ikiwamo vitabu pamoja na huduma za maabara ya sayansi.

Aidha, aliwapongeza walimu kwa kufanya kazi ya ziada ya ukaguzi wa wanafunzi na kuona wanapiga hatua kubwa ya maendeleo ya ufaulu.

"Matokeo ya wanafunzi waliofanya mitihani wa kidatu cha sita mwaka huu yanaonyesha kwamba ufaulu ni mzuri kwa asilimia 88.96 huku wanafunzi wakifaulu kwa daraja la kwanza hadi la tatu,"alisema.

Alifafanua kuwa matarajio katika mwaka 2020 ni kufanya vizuri zaidi katika daraja la juu na kuongeza ufaulu wa wanafunzi wa kuendelea na elimu ya juu vyuo vikuu na vinginevyo.

Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia taaluma, Madina Mjaka, alisema ufaulu huo umechangiwa zaidi baada ya kuondolewa kwa daraja la sifuri.

Aidha, aliwapongeza wanafunzi kwa kujiepusha na vitendo vya udanganyifu katika mitihani ambayo hupelekea kufutiwa kwa mitihani hiyo.

"Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imefurahishwa kwa wanafunzi kufanya mitihani ya kidatu cha sita bila ya kuwapo kwa matukio ya udanganyifu, "alisema

# Zungu awapongeza kuenzi utamaduni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKAZI wa jimbo la Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja wamepongezwa kwa kulinda na kuenzi utamaduni unaotokana na historia ya wazee wao, wenye umri wa zaidi ya miaka 60.

Ili kufanikisha zaidi ulinzi wa utamaduni huo, Mbunge wa Ilala, Mussa Azam Zungu, amewataka vijana kuiga wazee wao ili kudumisha na kulinda historia za taifa hasa mambo yanayounganisha jamii.

Alisema hayo wakati aliposhiriki katika sherehe za utamaduni wa "mwaka kogwa" huko Makunduchi mkoa wa Kusini Unguja.

Aliwapongeza wazee wa Kijiji cha Makunduchi kwa kuwa kwa zaidi ya miaka mingi sasa wamekuwa wakilinda na kutunza utamaduni wao ambao unatokana na historia na urithi kutoka kwa wazee wao.

Alisema ili utamaduni huo uweze kulindwa, vijana hawanabudi kufuata nyayo za wazee wao kuenzi na kutunza mila na utamaduni kwa ajili ya faida ya baadaye.

"Nimefurahishwa kumbe bado zipo familia zimekuwa zikilinda utamaduni wao ambao ni urithi kutoka kwa wazazi wao"alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Hassan Khatib, alisema faida kubwa za utamaduni na mila za "mwaka kongwa" ni kuukaribisha mwaka mpya na kujenga tabia ya kusameheana na kuvumiliana.

Alisema utamaduni wa mwaka kongwa ulianza zaidi ya miaka 60 iliyopita huku wananchi wa kijiji hicho wakijumuika na majirani zao katika kuadhimisha sherehe hizo za kijadi.

"Kijiji cha Makunduchi ndiyo pekee kwa hapa Zanzibar kilichofanikiwa kulinda utamaduni ambao wameurithi kutoka kwa wazazi wao"alisema.

Baadhi ya wazee wa Kijiji cha Makunduchi walifurahishwa kwa kuendelezwa na utamaduni huo wa kijadi ambao umerithiwa na vizazi vilivyopita.

"Nimefurahishwa na juhudi za wananchi wa kijiji cha Makunduchi wa kuenzi na kulinda utamaduni waliourithi kutoka kwa wazazi wao ambao ni heshima kubwa ya kijadi"alisema Abasi Juma mwenyeji wa kijiji hicho.

Sherehe za kijadi za mwaka kongwa hufanyika kila mwaka zikiwa ni ishara ya kuukaribisha mwaka mpya kwa ajili ya kuondosha nuksi na shari na kujenga upendo na mapenzi kwa wananchi wa kijiji hicho.



**JAGUAR ATUA BONGO KUMALIZA BIFU** Soma UK.15

JUMAMOSI JULAI 20, 2019

Nipashe MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE



# HOFU TUPU Irene Uwoya anamalizika hivihivi

BASI SAWA



## George amtukuza Mungu kwa uponyaji

MWIMBAJI wa muziki wa Injili, George Haule, ametambulisha albamu yake mpya inayoitwa 'Yote Ni Upendo Wako Mungu', kama shukrani kwa uponyaji aliofanyiwa.

Akizungumza na BT, Haule amesema wazo la kutoa wimbo huo unaobeba albam ni kumshukuru Mungwa kwa kumponya mtoto wake ambaye alikuwa akisumbuliwa na tatizo la figo.

"Siku moja nikiwa hospitalini namuangalia mwanangu akiwa akiwa ICU niliahidi kumuimbia bwana kama atapona, na mara miujiza ulipotokea niliamua kuandaa albam hii yenye wembo huu wa kumtukuza Mungu,"amesema George.



## Herimuziki kuja na 'Kolo' kimtindo

KILA kukicha muziki wa Bongofleva unazidi kupata zao jipya. Sasa kijana Herimuziki amekuja kuwabamba na aina ya kipekee wa muziki huo.

Hivi karibuni mwanamuziki huyo anayechipukia ametambulisha kibao chake kipya 'Kolo' chenye ladha ya muziki wa India na Bongo.

Wimbo huo umetayarishwa na prodyuza kimambo_na video yake imeongozwa na Joowzey chini ya kampuni ya Skylerk_don.



# HOFU TUPU
# Uwoya anamalizika hivihivi

KUFUATIA kufanya tukio la udhalilishaji kwa waadishi wa habari, msanii wa Bongo Muvi, Irene Uwoya, amekuwa na wakati mgumu wa kupokea simu kutokana na kuwa na hofu ya kushambuliwa.

Katika tukio hilo lililotokea mwanzoni mwa wiki hii jijini Dar es Salaam, Uwoya aliwatupia noti waandishi mara baada ya kumaliza kuzungumza kuhusu uzinduzi wa mtandao wa kuuzia filamu za wasanii.


Chanzo kilicho karibu na msanii huyo kimesema kwamba baada ya tukio hilo amekuwa mtu wa kupata hofu kila wakati pale anaposikia mlio wa simu yake ikiita.

"Irene anaonekana kuishi kwa hofu hata katika upokeaji wake wa simu, uenda hali hiyo ikamfanya ata kukonda katika kipindi iki,"alisema mtu wake wa karibu.

Katika Mkutano huo ulioitishwa na wana-Bongo Muvi wakiongozwa na mwenyekiti wao, Steve Nyerere, ulikuwa na lengo la kuzungumzia uzinduzi wa Swahiliflix ambao ni mtandao wa kuuzia muvi.

INSTA-TWITTER





Hivi na nyie kila kitu mnakishikia bango, vitu vingine changamsha genge tu. Mnapenda vita kuliko amani, hamjui kuvunga? Poleni! Mobetto Family tupo vizuri!! - **Amber Lulu.**



Mimi sijui ni mzaramo wa Soga na Maneromango? Naomba mtag mkondombwe na shoga king'ang'anizi **-Nagris Mohamed.**



# Kumbe Milly Manace alilelewa na JK

MSANII anayetamba kutoa 'cover' zinazovutia, Milly Manace, amesema Rais mstaafu Jakaya Kikwete, amesaidia kutimiza ndoto yake kwa kumsomesha.

Akizungumza hivi karibuni, Milly ambaye anatamba na cover ya wimbo wa Never Give Up, ulioimbwa na Harmonize, amesema kiongozi huyo alijitolea kumsomesha shule za mchepuo wa kiingereza hadi alipomaliza kidato cha nne.

"Namshukuru Jakaya Kikwete kwa moyo wake wa huruma hadi mimi nipo hapa, kipaji changu alikuwa akikijua na ndio maana alichukua jukumu la kunilea na kunipa moyo pale nilipokuwa na matatizo," amesema Milly.




**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

**@burudanitele**

## UNASEMAAA...

# Khadija Kopa awalilia wanaonyimwa kazi

MALKIA wa taarab nchini, Khadija Kopa, amewataka watu wanaoandaa matamasha ya burudani kuwaalika wasanii wa muziki huo ili waoneshe kazi zao.

Akizungumza hivi karibuni, Kopa amesema katika matamasha yanayoandaliwa nchini, yeye pekee ndiye anapata bahati ya kushiriki huku wengi wakiachwa.

"Namshukuru Mungu kwa upande wangu Napata kazi nyingi, lakini nyuma kuna wasanii wengi wanahangaika nawasihi watu wanaoandaa matamasha kuwajumuisha ili kazi zao zifiahamike," amesema Khadija Kopa.



## BODA 2 BODA

# Jaguar atua Bongo kumaliza bifu



MWANAMUZIKI na mbunge wa jimbo la Starehe nchini Kenya, Charles Kanyi, maarufu Jaguar ametua nchini Tanzania wiki chache baada ya kutoa matamshi ya uchochezi .

Kupitia akaunti ya Instagram Mbunge huyo alitupia picha ikionyesha yuko katika mitaa ya Dodoma na jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa BBC Swahili alisema kuwa amekuja Bongo kwa siku nne kuijulia hali familia yake mbali na kuwatembelea marafiki zake.

"Mimi naipenda Tanzania kwa sababu ni nchi nzuri na kama unavyojua nina kijana huku. Nawaambia Watanzania kwamba nawapenda sana na ndio sababu nimetembea hapa pia kama mtalii ili kuipatia kipato nchi hii", Jaguar

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Moja** ya kosa kubwa ambalo nimewahi kulifanya huko nyuma kwenye maisha yangu ni kuamini kuwa na nia nzuri na kufanya jambo zuri basi kila mtu anatakiwa akufurahie na akuunge mkono.Nilikuja kugundua siyo kweli. Unaweza ukafanya kila kitu kizuri na hao unaowafanyia bado wasione na wakakuchukia na ukabaki unashangaa kwa nini wanafanya hivyo-**Steve Nyerere.**



**Nafumba macho navuta hisia.** Naona dolla zinaning'inia. Nimeshachoka kusikilizia. Acha nisafiri hata kwa maji kama makinikia. Hata kibishi ninazamia.
Hata ndege nitadandia **- Kala Jeremiah.**



**Kwanza** huu uzi tu tayari (Arsenal) tushachukua makombe!! Uzi wakuendea disco kabisa!! Uzi matata kuliko vitimu vyote ulaya nzima **- Madee Ali.**

# Kuumbe!

## THE LION KING Tanzania imeipamba, Nigeria inapaishwa



WIKI hii Mwanamuziki maarufu wa Marekani, Beyonce, amefichua nyimbo zilizomo kwenye albamu yake mpya itakayoambatana na filamu mpya The Lion King.

Katika albamu hiyo ambayo imeitikisa dunia, ndani imejumuisha wasanii nyota wa muziki kutoka Afrika kutoka nchi ya Nigeria.

Wasanii hao ni Tiwa Savage na Mr Eazi wanatumbuzia katika wimbo wa 'Keys to the Kingdom', wengine Tekno na Yemi Alade katika kibao 'Don't Jealous Me'.

Burna Boy ana kibao cha kipekee au solo, 'Ja Ara E', huku msanii wa Cameroon Salatiel akionekana akiimba na Beyonce na Pharrell Williams katika kibao 'Water'. Wasanii wengine wa Afrika ni pamoja na Wizkid wa Nigeria, Shatta Wale wa Ghana, na Busiswa na Moonchild Sanelly kutoka Afrika kusini.

Kwa ujumla ndani ya albam hiyo, idadi kubwa ya wanamuziki walioshirikishwa ni kutoka nchi ya Nigeria na wachache kutoka Ghana, Mali na Afrika Kusini.

Katika jambo lilowashangaa wengi ni pale wasanii kutoka Afrika Mashariki hawajajumuishwa katika orodha hiyo, licha kutumika lugha ya Kiswahili na mandhari ya Mlima Kilimanjaro na mbuga ya wanyama ya Serengeti.

Ukiangalia kwa umakini wimbo wa 'Spirit' na filamu hiyo ya The Lion King, utagundua picha zote zimechukuliwa katika mbuga na mandhari ya Tanzania, lakini hakuna hata msanii mmoja kutoka ukanda huu aliyekanyaga zulia jekundu la filamu hiyo.

Alipotangaza mpango huo kwa mara aya kwanza wiki iliyopita, Beyonce alisema "Ilikuwa ni muhimu kuwa muziki usiimbwe na wasanii nyota na wenye vipaji bali iandaliwe na waandaaji wa Kiafrika. Ubora na moyo (mapenzi) vilikuwa vitu muhimu kwangu.

"Ni mchanganyiko wa kila kitu, si sauti moja tu. Kuna ushawishi kutoka kila kona, kutoka kwenye R&B, hip-hop na Afro Beat."

Inajumuisha pia vibao vya ushirikiano na wasanii wa Marekani kama Kendrick Lamar, Pharrell Williams, Childish Gambino, na binti yake Beyonce, Blue Ivy miongoni mwa wengine.

Ni kibao tofauti kilichotumika kuisindikiza filamu hiyo ya The Lion King, Spirit, chenye mistari ya kiswahili, hatahivyo kimejumuishwa pia kwenye albamu hiyo.

Wiki iliyopita, Beyonce aliachia kibao hicho kipya chenye maneno ya Kiswahili.


"Uishi kwa muda mrefu mfalme," sauti nyembamba inaimba kisha sauti nzito inaitika "uishi kwa", kionjo hiko kinajirudia mara mbili na kisha wimbo kuendelea kwa Kingereza.

Filamu mpya ya Lion King imetengenezwa na kampuni kubwa ya Disney nchini Marekani.





## Wazee wa 'bushi' Bongo Movie



BI MWENDA

**Na Adam Fungamwango**

KAMA nilivyoainisha wiki iliyopita kuwa kuna wasanii wana uwezo mkubwa wa kuigiza kwenye baadhi ya maeneo kuliko sehemu nyingine.

Tukawaangazia wasanii wa kike wenye uwezo mkubwa wa kucheza uswahilini, hasa wale wenye uwezo wa kusuta, na maneno ya shombo, mbwembwe na tashtiti.

Leo tutawaangalia wasanii ambao wakicheza maeneo ya vijijini wanaonekana kucheza kwa ustadi zaidi kuliko eneo lingine.

### MOHAMED FUNGAFUNGA 'MZEE JENGUA'

Pamoja na kwamba kuna wakati hucheza maeneo ya mjini, lakini ukitaka umfaidi zaidi acheze kama mkazi wa bushi.

Anajulikana kama ni mzee mtata, mkorofi, mkoloni, asiyetaka ushauri au kumsikiliza mtu yoyote kwa kile ambacho yeye anakiamini, kiwe kizuri au kibaya.

Akicheza shamba, wakati mwingine huwa kama mfalme, mtemi, baba, mwanakijiji au mchawi, huteka mashabiki wengi kutokana na aina yake ya uigizaji wa ukali uliopitiliza.

### FADHILI MSISILI 'MSISILI WA MSISIRI'

Ni mmoja kati ya wazee wenye uwezo mkubwa wa kuigiza hasa akiigiza akiwa kijijini.

Utampenda zaidi akiigiza kama mfalme au mtemi, lakini pia wakati mwingine huigiza kama mzee wa kijiji mwenye busara au baba wa familia.

Mzee Msisiri ana pande zote mbili. Anaweza kuigiza ukali au ukatili kama akiwa mtemi, lakini anaonekana kuwa na hekima na busara kama akiwa mzee wa kijiji au baba wa familia.

Mashabiki wengi wa filamu huwa hawapendi kumuona mzee huyu akipewa 'sini' za mjini.

### FATUMA MAKONGORO 'BI MWENDA'

Wengi wanamfahamu mama huyu kuwa ni mkorofi na mchawi. Ni kwa sababu watengenezaji wengi wa filamu wanaona anafaa sana kuigiza sehemu hizo na anavyoigiza analeta uhalisia zaidi.

Pamoja na yote hayo, Bi Mwenda anapendeza zidi akiigiza 'uchawi' wake akiwa kijijini zaidi kuliko mjini.

Na hata akiigiza kwenye 'sini' nyingine kama vile mama wa familia, utampenda zaidi akiwa kwenye mazingira ya bushi.

### HAMISI KORONGO 'MZEE KORONGO'

Kwenye tasnia ya filamu kumezuka baadhi ya wasanii wenye umri mkubwa wenye uwezo wa hali ya juu, kiasi cha wengine kujiuliza walikuwa wapi siku zote.

Mmoja wapo ni huyu mzee Korongo. Ni mzee mwenye kipaji cha hali ya juu kwenye uigizaji.

Anafiti kucheza maeneo yote ya mjini na kijijini, lakini ili umfaidi na kuona uwezo wake, basi awekwe kwenye 'sini' za kijijini, utampenda.

### ALLY NOGI

Huyu mzee utampenda sana ukiangalia filamu moja itaitwa 'Najua Kuoa'. Amecheza na Riyama Ally.

Hii ni filamu maarufu sana na hata wale waliokuwa hawamfahamu msanii huyu, wameanza kumfuhamu na kumfuatilia baada ya kuitazama hiyo.

Alicheza kama baba wa kijijini na mkewe Riyama, marehemu Mzee Majuto na wengineo.

Kutokana na kuicheza filamu hiyo kwa ustadi wa hali ya juu, hata wanaompa kazi nyingine ya kucheza filamu mara nyingi humtafutia mazingira yale yale ya kijijini ili kuufaidi uwezo wake Mzee Ally Nogi.

# Vijimambo

PICHA ILIYOPITA



1. Wanasema eti mimi chizi. Watanzania bwana kwa figisu! - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
2. Duuh! Jamani kazi kwanza, kuselifika baadae - Bahati, Kiwalani DSM.
3. Hii mitandao ya kijamii inatutesa. Kwa hii selfii kila mtu atakomenti 'nice' - Agatha Mbale, Moro Town.
4. Natafuta picha ya kutupia 'whatsap' - Dullah Dimoso, Tabata DSM.
5. Kijana hiyo simu imepitwa na wakati, ipeleke makumbusho - Oiso, Nyaishozi Tegeta DSM.
6. Ukisikia uchizi taslimu, basi ndio huo. Simu ya mezani na selfii! - Mama Nah, Manzese DSM.
7. Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.
8. Yes, hapa sasa pozi limekubali, ngoja nijifotoe sasa - Samwel Sungi, Utemini Singida.
9. Hii simu vipi, mbona sioni sehemu ya kujiselfisha? - Msabaha J. Msabaha, Mikindani Mtwara.
10. Lazima baby wangu aikubali hii picha, si selfii ya kitoto - Beneali Moussa Beneali, Migombani Zenji.
11. Hii inaitwa 'ekotite', muulizeni Kofi Olomide anaifahamu sana - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
12. Kweli ushamba mzigo. Wewe, sio kila simu unaweza kujiselfisha nayo - Mariam Beneali, Migombani Zenji.
13. Ha ha haaa, usitake ncheke mie! Hebu rudisha simu ya watu ofisini - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
14. Hapo 'chacha'! Disco limeingia watu wa kabila lileee! Mtajuta kuijua selfii - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
15. Mnashangaa nini? Mie sijiselfishi kama nyie, mie fundi simu jamani - Dully, Kiembesamaki Zenji.
16. Ukitaka kugombana naye, mwambie kuwa hiyo simu haiselfishi - Antar, Makumbusho Kijitonyama DSM.
17. Hapa sasa mademu wote wa 'bush stars' wangu - Nahoja Mazengo, Mbande Chamazi DSM.
18. Wewe! Hebu acha ushamba wako bwana, unawaabisha Wairinga wenzip - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
19. Hiyo selfii yako inanitia homa kwa kicheko - Bimkubwa Ausi Juma, Michenzani Unguja.
20. Hilo ndio tatizo la Wahehe wakishaingia mjini - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
21. Kaa hivyo hivyo, baada ya 'masaa' kadhaa utaona sehemu ya kupigia picha inajionyesha - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
22. Watu wa kizazi hiki, kweli wamedata. Haya bhana na selfii yako bandia - Mama Nah, Manzese DSM.
23. Kweli ushamba zigo la miba. Tangulini simu hiyo ikatumika kwa selifii? - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
24. Hiyo ni sawa na kuosha mchele kwenye mto wa maji mengi. Utapata taabu sana - Semeni Mpanjira, Kilwa.

**SMS Bomba ya Leo:**
**Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.**

PICHA MPYA



TUMA MESEJI - 0773 477 311




# Fitina: Mauti katika asali na maziwa

**Na Adam Fungamwango**



WAKATI mwingine mtu anaweza kuona anaonewa, au kunyimwa uhuru wake wa kuchagua kitu akipendacho. Kumbe inawezekana anaepushwa na mambo mabaya yanayoweza kumpata mbele ya safari.

Kizazi cha sasa kimekuwa kikibeza tabia ya kuchaguliwa wenza au wachumba na kusema ni mambo ya kizamani ambao imepitwa na wakati.

Ni kweli, lakini pia vijana wa kizazi cha sasa inabidi wawasikilize pia wazazi wao au wakubwa zao juu ya watu wanaotaka kuwa wenza wao kwa sababu mara nyingi wanajua vitu vingi vilivyojificha kuliko vijana.

Ukiingalia filamu ya 'Fitina', inawafundisha vijana juu ya kutafuta ushauri kwa wakubwa wanapotafuta wachumba na kama watakakaa wasilazimishe, bali ni kukaa nao ili kujua sababu na si kukurupuka na kuwaona kama wana chuki au wamepitwa na wakati.

Wahusika kwenye filamu hii kwa majina yao ya kazi ni Mze Nzonzo, Logolo, Mtumuyu, Okela, Ngwele, Zimbwe, Fitina, Siwatu, Mandae, Kipongo, Enika na wengineo.

Fitina ni binti mmoja anayewazidi wasichana wengi urembo kwenye kijiji anachoishi. Wanaume wengi wanajitokeza kutaka kumuoa, lakini inashindikana kutokana na kuwa na nyodo.

Hata hivyo, kuna wachumba wawili maarufu kijijini hapo ndiyo walileta kashehe. Wa kwanza ni Okelo, kijana mtanashati kijijini hapo na Nzonzo, mzee mwenye umri kubwa, lakini mwenye mali nyingi kijijini.

Mandae, shoga yake Fitina, anamshauri aolewe na mzee Nzonzo kwa sababu ana mali nyingi, nyumba, mashamba na rasilimali nyingine, ili hata akifa yeye na watoto wake waweze kurithi mali, tofauti na kuolewa na Okelo asiye na kitu chochote, zaidi ni kujidai naye tu mitaani.

Baada ya ushauri na muda mrefu, Fitina anaamua kufuata ushauri na shoga yake na kuamua kuwa na mzee Nzonzo, huku akimpiga 'kibuti laivu' Okelo.

Baba mzazi wa Fitina, mzee Kipongo yeye alipenda zaidi binti yake aolewe na kijana Okela na si Kipongo kwa sababu umri wa mzee huyo ni sawa na wa kwake tu.

Mzee Nzonzo na yeye akaamua kuwa mbogo kwa yoyote anayeonekana kutaka kuvuruga penzi lao, licha ya kwamba baba mtu hataki amuoe.

Okela naye anatumia ukaribu wake na 'mkwewe' Kipongo kutaka kumuoa Fitina. Kijiji kinagawanyika sehemu mbili, kila mwanakijiji na upande wake na sababu zake.

Kizaazaa kinaanza, patashika nguo kuchanika. Kijiji hakikaliki, ugomvi moja kwa moja. Baba kila siku akawa na kazi ya kwenda 'kumchomoa' binti yake nyumbani kwa mzee Nzonzo, lakini kesho yake anarudi tena.

Kikao kikubwa kikafanywa kijijini hapo baada ya hali ya usalama kuwa mbaya na kuhudhuriwa na watu wote kijiji. Baba Fitina akatapika nyongo kuwa tatizo analokataa binti yake Fitina asiolewe na mzee Nzonzo si kwa sababu ana umri mkubwa na binti yake ana umri mdogo la hasha.

Ina ni historia ya mzee Nzonzo kwani kila anapooa, mkewe anafariki baada ya mwaka mmoja. Na tayari wake zake 12 wameshafariki, hivyo anajua binti yake akiolewa ni lazima atakufa na kuwa wa 13. Hiyo ikawafumbua macho baadhi ya wanakijiji waliokuwa hawajui, akiwemo Fitina mwenyewe.

Nzonzo alikiri hilo na kusema hata yeye haelewi sababu, ila alitaka kumuona Fitina amzalie watoto wawe warithi wake kwa sababu hana mtoto hata mmoja. Baada ya hapo mzee Nzonzo akaamua kilio na kubembelezwa na Baba Fitina mzee Kipongo japo walikuwa haelewani.

Kwa kauli yake kwenye mkutano, Nzonzo alitamka kuwa anaahirisha mpango wake wa kutaka kumuoa Fitina na anamuachia kijana Okelo na harusi hiyo ataigharamia yeye mwenyewe mzee Nzonzo.



## FEDHA UTOTONI

# Kross awa bilionea mtoto

MTOTO Kross Asghedom, pengine ataingia katika orodha ya matajiri baada ya mahakama kuridhia apewe Sh. Bilioni mbili.

Tukio hilo linakuja baada ya miezi mitatu kupita tangu baba yake rapa maarufu wa Marekani Nipsey Hussle kufariki dunia.

Kross Asghedom alizaliwa na muigizaji Lauren London ambaye alikuwa mchumba wa mwanamuziki huyo ambaye aliuawa kwa kupigwa risasi.

Pesa hizo zimetolewa kama huduma ya uhifadhi 'Guardianship' kwenye urithi wa baba yake.

Kwa mujibu wa nyaraka zilizohifadhiwa na mtandao wa The Blast umeripoti kuwa mama mzazi wa mtoto huyo Lauren London amefungua faili kwa ajili ya kuhakikisha mwanae huyo mwenye umri wa miaka miwili anakuwa na usalama na maisha yake.

Imeripotiwa kuwa kwenye faili hilo Lauren amekiri kwa kuandika kuwa kwa sasa ana jukumu la kuwalewa watoto wote aliowaacha Nipsey na anapenda kuwa mlezi wa mwanae katika kumsimamia masuala ya kisheria ikiwemo mali alizoacha Nipsey.

na imeelezwa kuwa Lauren alimuandikisha mtoto wa kwanza wa Nipsey, Emani'10 kama ndugu wa Kross.

Mauaji ya Rapper Nipsey Hussle yaliyotokea March 31,2019 nje ya duka lake la 'The Marathon Clothing' mjini Los Angeles na alizikwa April 12, mwaka huu katika makaburi ya Forest Lawn Memorial Park yaliyopo Hollywood Hills.

Kutokana na ukwasi huo wa fedha, mtoto huyo anatajwa kuwa miongoni mwa matajiri wadogo katika nchi hiyo.



# Wizkid usizuge, kubali yaishe

BAADA ya Wizkid kushutumiwa kwa unyanyasaji wanawake, mwanamuziki huyo amejaribu kutuliza hali ya hewa kwa kuposti mtandaoni picha ya mtoto wake wa tatu.

Hivi karibuni msanii huyo amekuwa akilaumiwa kwa kumnyanyasa mama wa mtoto wake huyo Jada Pollock kwa kumpa kipigo.

Hata hivyo kwa kutumia akaunti yake ya Instagram, Wizkid ameweka picha yake akiwa na mtoto wake huyo akionyesha kwamba anajali familia yake.



## Kim, Trump wamjadili Asap kifungoni

MWANAMITINDO na mke wa rapa, Kanye West, Kim Kardashian, ametinga ndani ya Ikulu ya Marekani kwa lengo la kumsaidia mwanamuziki Asap Rocky atoke kifungoni.

Kwa mujibu wa mtandao wa TMZ Kim pamoja na mumewe Kanye West wako katika harakati kubwa ya kumpigania msanii huyo kwa Rais Donald Trump kusaidia kutoa jela.


Rapper huyo kwa sasa amefungwa nchini Sweden, lakini Kim na Kanye wamefikia hatua nzuri baada ya kukutana na mkwe wa Trump ambaye ni Jared Kushner na alimuelezea kuhusu kesi ya Asap.

## Nas atangaza ujio The Lost Tape 2

RAPA mkali wa Marekani, Nas ameendelea kutoa muendelezo wa album yake ya 'The Lost Tape 2' ambayo inatarajia kuachiwa rasmi July 19, mwaka huu.

Inaripotiwa kuwa wakati wa sherehe ndogo iliyoandaliwa na mkali huyo kwa ajili ya kusikiliza ngoma zilizopo ndani ya Album ya 'Lost Tape 2', Nas aliamua kufunguka mbele ya marafiki zake na kuweka wazi kuwa tayari ana ngoma za kutosha tu kwa ajili ya Album ya The Lost Tape 3 na 4.

Album ya 'The Lost Tape 2' ni muendelezo wa toleo la kwanza ambalo aliiachia mwaka 2002 album hiyo imeandaliwa na Pharrell, Swizz Beatz, RZA, No I.D., Hit-Boy, Pete Rock na Kanye West.





## Yemi Alade ashukuru Mungu kwa yote

MWANAMUZIKI wa Nigeria,Yemi Alade, amekuwa miongoni mwa wasanii wenye furaha baada ya kuwamo katika albamu mpya ya Beyonce inayojulikana kamma 'Lion King.'

Katika uzinduzi wa filamu inayobeba jina la wimbo huo, Yemi Alade alijiunga na wasanii wengine kukutana na Beyonce na kisha kuzungumza naye.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram, Yemi Alade alishiriki kwenye video hiyo na kuandika "Nimekutana na malkia, namaanisha,Oops namaanisha Beyonce," ameandika.

## Babu Kevin una bahati kweli

MUONGOZAJI wa filamu Marekani, Kevin Spacey, ameshinda kesi yake ya jinai na kuwabwaga waendesha mashtaka ambao walitaka kesi hiyo iendelee kusikilizwa.

Kulingana na TMZ, makala iliyotumika kama ushahidi wa kumtia hatiani ilikataliwa na mahakama kutokana na kutokidhi ukweli wa mashtaka yanayomkabili.

Pia imearifiwa kwamba waathirika hawakuweza kuishawishi kuwa kesi ya jinai na hata waendesha mashtaka walipojaribu kutetea walishindwa.



SAFU



Na John Juma
0716217615

## Mionzi ya Sheria

# Mwongozo ukoje pale mteja anaposhindwa kurejesha Mkopo?

MASUALA ya kuweka mali rehani ili kupata mkopo hapa nchini yanaongozwa na sheria kuu mbili nazo ni Sheria namba 4 ya Ardhi ya mwaka 1999 sura ya 113, pamoja na sheria namba 17 ya rehani ya mwaka 2008.

Kifungu cha 127 (1) cha Sheria ya Ardhi, kinatambua habari ya mhusika kushindwa kurejesha mkopo. Kinaielezea hatua hiyo kama miongoni mwa mambo ambayo yanakiuka masharti ya mkataba wa mkopo.

Wiki iliyopita tulianza sehemu ya kwanza ya makala hii na sasa tumalizie vipengele muhimu vya kuzingatia kwenye masuala ya rehani.

Ukiukaji wa masharti ya mkopo kutumia mali iliyowekwa reheni inaweza kuwa ni pamoja na kuweka mali hiyo reheni kwa taasisi au mkopeshaji zaidi ya mmoja.

Aidha, kuuza, kupangisha bila ya hata mhusika kutoa taarifa au kuomba ridhaa kwanza kutoka kwa mtoa mkopo nao ni ukiukaji.

Hata hivyo haya na mambo mengine yanayofanana na hayo yatachukuliwa kama kukiuka masharti ya mkopo ikiwa yamekatazwa, wazi wazi, katika kupitia mkataba baina au kati ya taasisi ya fedha na mteja wake.

Pia kwa mujibu wa sheria mteja kushindwa kurejesha mkopo kunajumuisha pesa kamili aliyoiweka kama mkopo, riba, pamoja na makato mengine ambayo na yenyewe yanafanya sehemu ya mkopo huo.

**NOTISI SIKU 60**

Notisi ni ya lazima kabla nyumba au kiwanja cha mteja hakijauzwa. Bado siyo tu lazima mhusika kupatiwa mapema, bali pia ni matakwa ya kisheria kutoa muda wa siku zisizopungua 60.

Hivyo basi, mtindo wa kutoa au kuwapatia wahusika notisi ya siku 14 tu au wakati mwingine chini hizo ni kukiuka taratibu za kisheria zilizowekwa.

Kifungu cha 127(1) (a) cha Sheria ya Ardhi kinaeleza kuwa pale mkopaji anapokuwa ameshindwa kurejesha mkopo kwa wakati au kwa mujibu wa makubaliano ya awali, basi taasisi ya fedha itampatia mkopaji, au mteja wake taarifa ya siku 60 juu ya nia yake ya kuuza mali.

Siku hizo zikiisha kabla mkopaji hajalipa moja kwa moja taasisi hiyo itaweza kuendelea na hatua za kuuza ikiwa tu itaamua kufanya hivyo. Kimsingi, ni lazima mteja apatiwe taarifa ya siku 60 kabla.

Siku hizo zinaanza au zitaanza kuhesabika kutokea siku taarifa ilipopokelewa au kumfikia mteja. Kinyume chake itakuwa ni kosa kwa mujibu wa sheria.

**MUHIMU**

Notisi haishii kuhusika tu pale mteja anaposhindwa, atakaposhindwa kufanya malipo kwa mujibu wa makubaliano.

Bali pia kufuatia ukiukwaji wa sharti lolote lile la haki katika mkataba wa mkopo, ambalo taasisi ya fedha inadai mteja wake amelikiuka.

Hapo pia, katika mazingira kama hayo, itabidi mteja husika kuchukuliwa hatua kisha taratibu nyingine baada ya hiyo zitafuatia.

**UKIUKAJI NOTISI**

Awali ya yote, kama nyumba au kiwanja bado hakijauzwa nenda mahakamani ili kuweka zuio (Caveat); na piliendapo mali imeshauzwa bado mhusika anaweza kufungua shauri mahakamani kubatilisha mauzo hayo batili kwa msingi wa kukiukwa kwa taratibu nzima za mauzo, na kurejeshewa mali yake.

**ANGALIZO**

Kwa mujibu wa Sehemu ya (iii)-Kanuni ya 7(1), Kanuni mpya za Sheria ya Ardhi kupitia tangazo la Serikali namba 345 la Aprili 2019.

Inaelekeza, mwenye kiwanja au shamba ambalo (kwa namna moja au nyingine) halijaendelezwa au lenye maendelezo hafifu ikiwa ataomba mkopo na kuweka rehani ardhi hiyo, atatakiwa ndani ya miezi sita kutokea siku alipoweka rehani, apeleke taarifa kwa kamishna wa ardhi kuonyesha ni namna gani pesa yote au sehemu ya pesa alizokopa zimetumika katika kuendeleza ardhi hiyo.

Hili ni kwa ardhi zilizopimwa pekee, majanga kwa wamiliki wasio rasmi. Mfano kama taasisi ya fedha (benki) itaamua kukupatia mkopo kwa 'sharti kuu' la kuliendeleza eneo husika basi ndani ya miezi sita tokea mteja apokee mkopo ni lazima atawajibika kutimiza takwa la kutii kupeleka au kuwasilisha 'taarifa maalum' kwa Kamishna wa Ardhi.

Ataonyesha ni kwa namna au jinsi gani mkopo huo umetumika kuendeleza ardhi ambayo imetajwa kama rehani, hata kama mkopo husika unatoka kwa mafungu (installments).

Aidha hata kama hizo fedha zinakopwa maalum kwa ajili ya kuanzisha au kuendeleza biashara fulani, kununua gari ni lazima kiasi fulani kitengwe kwa ajili ya kuiendeleza ardhi inayohusika.

Na taarifa ya namna pesa ilivyotumika kuendeleza eneo itatakiwa kutolewa katika fomu maalum ambayo imeanzishwa na Sheria ya Ardhi fomu namba 551.

Zaidi, udanganyifu wowote katika mchakato mzima ni jinai inayoweza kupelekea mhusika (yeyote) kwenda jela kwa kifungo kisichozidi miaka miwili au faini, ama vyote viwili kwa pamoja, kwa mujibu wa kanuni ya 9 ya sheria ya reheni.



Reubeni Lumbagala

## Kalamu ya Mwalimu

# Tuusikie mwenge tutunze mazingira

MWENGE wa uhuru unaendelea kukimbizwa katika maeneo mbalimbali ukizindua miradi ya maendeleo na kutoa elimu ya uraia kwa wananchi.

Kauli mbiu ya mbio hizo kwa mwaka huu wa 2019 ni "maji ni haki ya kila mtu. Tutunze vyanzo na tukumbuke kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa".

Mbio hizi za mwenge ni muhimu kuendelezwa kutokana na umuhimu wake katika kuchagiza maendeleo kwa kuzindua miradi ya maendeleo na kuzungumzia masuala mbalimbali yenye tija kwa taifa na kutoa elimu kwa wananchi.

Sekta ya mazingira ni muhimu katika upangaji wa maendeleo. Bila kuwa na mazingira bora, juhudi za kimaendeleo zitakwama. Changamoto kubwa inayoikabili sekta ya mazingira ni kukosa utunzaji kutoka kwa wananchi wenye jukumu la kuyalinda ili kuwapo na ustawi na maisha ya binadamu na viumbe hai wengine. Hivyo, juhudi kubwa zimekuwa zikifanywa na serikali pamoja na wadau wengine wa mazingira katika kuhakikisha Tanzania inaendelea kuwa sehemu salama ya kuishi kwa kutunza mazingira kwa maendeleo endelevu ya vizazi vya sasa na vya baadaye.

Kauli mbiu ya mbio za mwenge mwaka huu, imebeba ujumbe wa elimu kwa umma juu ya masuala mawili yaani utunzaji wa mazingira na uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba mwaka huu. Makala hii inaangazia eneo la utunzaji wa mazingira lililobebwa katika kauli mbiu ya mwenge wa uhuru. "Maji ni haki ya kila mtu. Tutunze vyanzo vyake", hii ni sehemu ya ujumbe uliopo katika kauli mbiu hiyo ambayo inasomeka kwenye mikoa yote mwenge unapopita.

Maji ni uhai. Upatikanaji wa maji safi, salama na yenye kutosheleza unategemea namna mazingira yalivyotunzwa na kuhifandhiwa.

Bila kutunza vizuri mazingira pamoja na vyanzo vya maji, usambazaji wa huduma ya maji kwa wanachi utakwama kwani upatikanaji wa maji hautakuwa wa uhakika na hivyo kukwamisha juhudi za kuwafikishia wananchi huduma hiyo muhimu kwa matumizi ya viwandani na uzalishaji.

Wananchi ambao ni watumiaji wa maji wana wajibu wa kutunza mazingira ili maji yawafikie wale ambao bado hayajawafikia na huduma ya hiyo .

Viongozi wa mbio za mwenge wanapoendelea na shughuli zao za uzinduzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo, hutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na umuhimu wa wao kuwa mstari wa mbele kutunza mazingira ili kila mwananchi aweze kupata huduma ya maji.

Maji yataendelea kububujika kutoka katika vyanzo vyake kama vyanzo vya maji hayo vitatunzwa kikamilifu. Wananchi wahakikishe wanatoa taarifa kwa vyombo vya ulinzi na usalama kwa wale wanaofanya shughuli za kibinadamu katika vyanzo vya maji.

Wapo wananchi wanaoendesha shughuli za kilimo na ukataji miti karibu na vyanzo vya maji ambavyo vinawahudumia wananchi wengi katika kuwapatia maji. Pamoja na ukweli kuwa wananchi wanayo haki ya kujishughulisha na shughuli za kiuchumi ili kujenga nchi, lakini ni muhimu shughuli hizo zisivunje sheria za nchi.

Mwendelezo wa shughuli hizo za kilimo na ukataji miti kwa ajili ya mbao na kuni, ni kuharibu vyanzo vya maji na kusababisha wananchi kukosa huduma muhimu ya maji.

Maji yanahitajika sana kutokana na umuhimu wa wananchi kushiriki kilimo cha uhakika cha umwagiliaji ili kuwa na uhakika wa kuvuna badala ya kutegemea kilimo cha mvua.

Upatikanaji wa maji ukiwa wa kusuasua, utakwamisha juhudi za serikali za kuhamasisha wananchi kutumia kilimo cha umwagiliaji. Maji yakiwa hayapatikani au hayatoshelezi, itakuwaje kuhusu uanzishwaji wa kilimo cha umwagiliaji.

Maji pia ni bidhaa muhimu katika shughuli za viwandani kwani yanahitajika sana katika utengenezaji wa bidhaa mbalimbali na kwa matumizi ya huduma kuanzia hospitalini, shuleni na kwenye hoteli na migahawa.

Kuharibu mazingira ambapo kutasababisha uhaba wa maji ni kurudisha nyuma juhudi za serikali za ujenzi wa viwanda na kuzalisha uchumi.

Haya yote yanathibitisha namna ambavyo mazingira yanapaswa kulindwa kwa nguvu zote na kila mwananchi ili mipango mbalimbali ya kimaendeleo iweze kutekelezeka kwa urahisi.

Kabla ya wananchi kulalamikia ukosefu wa maji katika maeneo yao, wanapaswa kujiuliza kwanza juu ya ushiriki wao katika utunzaji wa vyanzo vya maji na mazingira kwa ujumla.

Hakuna namna ambayo wananchi wanaweza kupata maji safi, salama na yenye kutosheleza kama vyanzo vya maji vitaharibiwa na wao wenyewe.

Hivyo basi, wananchi wazingatie elimu inayotolewa na viongozi wa mbio za mwenge kuhusiana na utunzaji wa vyanzo vya maji na mazingira ili kila mwananchi aweze kufaidi huduma ya maji.

Wote wanaohujumu sekta ya mazingira na vyanzo vya maji wachukuliwe hatua kali ili kuwa fundisho kwa wengine wanaocheza na uhai na maisha ya binadamu kwa kuharibu mazingira.

Kongole Mwenge wa uhuru, 2019 kwa kumulika utunzaji wa mazingira. Tafakari.

# Taasisi yawafungulia milango Watanzania kusoma ng’ambo

Na Marry Geofrey



Wahitimu wa vyuo vikuu wakifurahia mafanikio. **PICHA: MTANDAO.**

KATIKA jitihada za kunyanyua elimu nchini kumekuwa na mbinu mbalimbali ambazo zinatumiwa na taasisi za serikali na zisizo za umma kuboresha ili kufikia azma hiyo.

Zote zikiwa na lengo la kuhakikisha elimu inakuwa imara, bora na endelevu.

Pamoja na jitihada hizo za serikali na taasisi nyingine kuboresha elimu nchini, inaonekana wazi kuwa wazazi wengi wanapenda kuwapeleka watoto wao nje ya nchi kusoma wakiamini kuwa huko kuna mazingira mazuri na elimu bora zaidi.

Hakuna asiyefahamu kwamba kuwapo na elimu na mazingira bora ya kumvutia mwanafunzi kusoma ndipo kutamfanya aweze kufaulu vyema masomo yake na kuipenda shule.

Katika kuliona hilo, Kampuni ya Global Education Link inayofanya kazi ya kuwatafutia wahitimu nafasi za kwenda kusoma katika vyuo vya nje ya nchi, inaeleza kuwa itaendelea kuifanya kazi hiyo kwa weledi.

Regina Lema ni Meneja wa Tawi la kampuni hiyo mkoa wa Dar es Salaam, anasema tangu kampuni hiyo ilipoanzishwa mwaka 2016 mpaka sasa imefanikiwa kuwapeleka wanafunzi zaidi ya 5000 nje ya nchi kwenda kusoma.

Lema anasema mwitikio wa wanafunzi kwenda kusoma nje ya nchi umekuwa mkubwa jambo ambalo limesaidia kuongezeka kwa wataalam wengi nchini.

Anasema mwitiko huo pia unatokana na ufaulu mzuri wa wanafunzi hao waliopata nafasi ya kusoma nje ya nchi.

Lema anasema kampuni yao imekuwa kiwafuatilia wanafunzi hao wanaokwenda kusoma nje kuanzia hatua ya ushauri, pamoja na kupita mashuleni kutoa elimu juu ya kozi gani wanaweza kusoma chuo kikuu.

“Sisi tumekuwa tukiwafuatilia wanafunzi wetu huku nje ya nchi wanapokwenda kusoma lakini pia wanapohitimu masomo tunaendelea kuwashauri pia,” anasema.

Anaeleza kuwa kila mwanafunzi anayechagua chuo cha kusoma nje ya nchi kupitia kampuni yao humfanyia mchakato wa udahili, utafutaji wa visa, hati ya kusafiria pamoja taaratibu nzima ya vibali vya serikali.

“Baada ya hapo sisi pia tunafanya mchakato wa kumtafutia tiketi na mara nyingi wanafunzi wetu hutumia ndege moja kusafiri unakuta wanafunzi 50 wanasafiri kwa pamoja wakiwa na wafanyakazi wetu wanne,” anasema.

Anaeleza kuwa wanafunzi hao baada ya kufika huko huwapeleka hadi chuoni na wakishaanza masomo ndipo wafanyakazi hao wanarejea nchini kwa ajili ya shughuli zingine.

Lema anasema ili kujua anachokifanya mwanafunzi akiwa masomoni, wanamfumo maalum ambao humfatilia kwa kuangalia matokeo yake ya mtihani, majaribio pamoja na mwenendo mzima wa maisha yake.

“Kipo pia kitengo kingine ambacho kazi yake ni kuhakikisha wanafatilia maendeleo ya siku kwa siku ya wale wanafunzi yaani namna wanavyofanya kazi zake darasani, kuchukua matokeo na kuwapatia wazazi na masuala mbalimbali ya kijamii wanayoyafanya huko,” anasema.

Kadhalika, pia wanao umoja wa wazazi wa wanafunzi wanaosoma nje ya nchi ambao umekuwa ukituma mwakilishi kuzunguka nchi mbalimbali ambazo wanafunzi hao wanasoma kwa lengo la kuangalia mienendo ya watoto wao.

**KUHUSU MAHAFALI**

Akizungumzia mahafali, Lema anasema mwaka huu kampuni hiyo kwa mara ya kwanza itafanya mahafali ya kwanza ya wanafunzi waliosoma nje ya nchi kwa lengo la kuwahamasisha wanaoendelea kusoma kwa bidii na hao waliomaliza huwaunganisha na fursa za ajira.

“Wanafunzi hawa wameshamaliza kusoma huko nje na kufanya vizuri sasa wanarudi nyumbani wanafanyiwa mahafali mengine, hii tunaimani itawasaidia waliopo masomoni kujitahidi kusoma kwa bidii ili waje kuwasaidia wazazi,” anasema Lema.

Mahafali hayo ambayo yanatarajia kufanyika Agosti 11 mwaka huu yatawakutanisha wahitimu hao na waajiri ambao wanaamini watapata fursa ya kuwaona vijana hao namna walivyokuwa bora kisha kupendezewa kuwaajiri.

“Waajiri watakuwepo hivyo itakuwa ni rahisi kwao kuwapata watu wa taaluma mbalimbali waliosoma nje ya nchi, lakini pia wanafunzi hawa wataandika na kuandaa project zao ambazo zitawasaidia na wao pia kama wakipata watu wa kufanya nao kazi,” anasema.

Anasema kwa sasa kampuni hiyo imetanuka kutoka kuwapo katika mkoa mmoja hadi kwenye mikoa mingine mitano ambayo ni Mwanza, Arusha, Dodoma, Mbeya na Zanzibar.

**CHANGAMOTO**

Meneja wa Tawi la Dar es Salaam, anasema moja ya changamoto wanayokumbana nayo ni uelewa mdogo wa wanafunzi kuhusu kozi anayotaka kwenda kusoma jambo linalochukua muda mrefu kumuelewesha.

“Hii ni changamoto ambayo tunakumbana nayo, unakuta mtu anapomaliza kidato cha sita ndipo anaanza kufikiria cha kusoma jambo ambalo halitakiwi, “ anasema Lema. Na ili kukomesha jambo hili tumekuwa tukizunguka mashuleni kutoa ushauri kwa wanafunzi na kuwaeleza ni kozi gani anaweza kusoma pindi anapomaliza elimu yake ya Sekondari” anasema Meneja Lema.

Anaeleza kuwa kwa miaka ya nyuma pia walikuwa wakikumbana na changamoto ya wazazi na wanafunzi kufikiri kuwa kwenda kusoma nje ya nchi ni gharama kubwa.

“Miaka ya nyuma changamoto hii ilikuwa kubwa sana ila sasa hivi tunashukuru inapungua kwani tunawaelewesha watu kuwa upo mkopo usiokuwa na riba ambao mzazi anaweza kukopa na kwenda kumsomesha mtoto wake nje ya nchi,” anasema.

Lema anasema changamoto nyingine ni kuchelewa kutoka kwa matokeo ya kidato cha sita hapa nchini hali inayochangia shughuli za kumfanya mtoto kwenda kusoma nje ya nchi kufannyika kwa muda mfupi.

“Matokeo yanachelewa sana kutoka hivyo inamlazimu mtoto kutumia muda mfupi kufanya udahili wa kusoma nje ya nchi na hii inakuwa mzigo hata kwa mzazi kwakuwa wanakuwa hawajajiandaa,” anasema.

**MALENGO YAO**

Lema anabainisha malengo yao ni kuwa moja ya mawakala wakubwa duniani wanaowatafutia wanafunzi vyuo vikuu nje ya nchi vyenye ubora wa hali ya juu.

“Pia lengo letu si tu kuwapeleka watu kwenda kusoma nje ya nchi tunategemea na wenzetu huko waje hapa nchini ili na wao waweze kusoma na kwa kulitekeleza hilo tayari tumeshafungua ofisi zetu China, Zambia na tunawakala Kenya,” anasema Lema.

Aidha, lengo lao jingine ni kuhakikisha jamii inaelimika hivyo watajitahidi kwa hali na mali wanafunzi wapate elimu bora.

**WITO**

Meneja Lema anatoa wito kwa wahitimu wote wa elimu ya sekondari kutembelea kampuni hiyo kwa lengo la kupata ushauri kuhusiana na chuo gani anaweza kusoma nje ya nchi.

“Tunafanya kazi na vyuo zaidi ya 500 nje ya nchi hivyo wanafunzi wasisite kututembelea ili kupata ushauri au maelekezo.” Anasema Lema.

MAKALA

# SIMANZI NAOMI

## ■Ndugu wasubiri kipimo DNA
## ■Ikithibitika kuzikwa kwa heshima

**Na Beatrice Moses**

MAPENZI yanaua. Ni msemo ambao unaweza kuhusishwa na matukio kadhaa na visa vya mauaji vinavyotokana na migogoro ya uhusiano wa mapenzi wakiwamo walio kwenye ndoa.

Kisa cha mauaji kinachotajwa kumkuta mwanandoa Naomi Marijani, (36) ni cha kusikitisha ambapo kwa hakika kimeacha maswali kadhaa ambayo ni kitendawili kinachongoja mahakama kukitegua.

Ni wazi kwamba ndugu, jamaa na marafiki kama wanajamii wanalazimika kusubiri mahakama kutoa maelezo iwapo Naomi mama wa mtoto mmoja ameuawa na mumewe anayetajwa kwa jina la Khamis Luongo,(38).

Inasubiriwa korti iufahamishe umma, kwa nini aliamua kumteketeza kwa mkaa na kufanya majivu yake mbolea ya mgomba.

Ni kwa nini alimshitaki mkewe kuwa ametelekeza mtoto wao wakati akijua kuwa ameshamuua?

Hayo ni miongoni mwa maswali ambayo Luongo atakapandishwa kizimbani anatarajiwa kuyajibu baada ya mahakama kumsikiliza na kujuua ukweli.

Zaidi kufahamu ni kipi kilimchochea kufanya mauaji hayo yanayoshangaza na kufikirisha wengi.

**MAELEZO YA POLISI**

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Temeke, Amon Kakwale, anazungumzia tukio hilo, akibainisha kuwa asubuhi ya Mei 15 mwaka huu, katika eneo la Gezaulole Wilaya ya Kigamboni jijini Dar es salaam, Luongo, anashukiwa kumuua mkewe.

"Mara baada ya mauaji hayo Luongo anaeleza kwamba alichukua mwili wa mke wake na kuuweka kwenye shimo alilolichimba kwenye banda la kufugia kuku kisha aliweka mkaa magunia mawili na mafuta ya taa akawasha moto," anasema Kamanda.

Luongo anatajwa kuwa ni mfanyabiashara, inayeelezwa kuwa baada ya kuuteketeza mwili huo alichukua mabaki kwa gari lake lenye namba T 206 CEJ aina ya Subaru Forester.

Aliyapeleka shambani kwake kijiji cha Mlogolo huko Vikindu Wilaya ya Mkuranga Mkoa wa Pwani na kuyazika, kisha akapanda mgomba juu yake.

Kamanda anabainisha kuwa baada ya kufukia majivu na kupanda mgomba alirudi nyumbani kwake akitangaza kuwa mke wake ametoroka nyumbani.

**KUBAINIKA**

Kakwale anasema siku nne baadaye, ilipofika Mei 19, Luongo alifungua jalada polisi kuwa mke wake ametoroka nyumbani na kupewa RB yenye kumbukumbu MJ/RB/234/2019 kutoka kituo kidogo cha Polisi Mjimwema.

"Baada ya kufanya hayo inaelezwa kuwa Luongo aliwajulisha ndugu jamaa na marafiki zake kuwa mke wake ametoroka nyumbani. Juni 12, mwaka huu alifungua jalada jingine KGD/IR/3617/2019 linalomlalamikia mkewe kumtelekeza mtoto, aitwaye Gadious Khamis mwenye miaka sita," anasema Kamanda Kakwale.

**HOFU YA NDUGU**

Kamanda Kakale, anaongeza kuwa ndugu wa Naomi nao walifungua jalada katika kituo cha Temeke Juni 13 mwaka huu, kutoa malalamiko ya kupotea kwa ndugu yao wakiomba kufanyike uchuguzi.



"Upelelezi uliendelea. Luongo akiwa anaenda kuripoti Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi (RCO) Temeke hadi tarehe 15 Julai mwaka huu alipozuiliwa kwa mahojiano ya kina ndipo akaamua kusema ukweli kuwa alimuua mkewe."

Yanayodaiwa kuwa ni mabaki ya mwili wa Naomi yalipatikana Julai 16 mwaka huu, huko shambani kwao, baada ya polisi kuelezwa kuwa ndiko eneo yalipozikwa.

Taarifa kutoka kwa ndugu wa Naomi zinabainisha kuwa ununuzi wa gari la mtumba aina ya Vitz unaweza kuwa sababu ya mauaji ya ndugu yao huyo.

Akizungumza na Nipashe kaka wa marehemu Wiseman Marijani, anasema kuwa Luongo alikuwa na mgogoro na mkewe baada ya kuona amenunua gari hilo bila kumwomba fedha.

Anaeleza kuwa Naomi alinunua gari hiyo baada ya kuchukua mkopo kutoka kwenye fedha zinazotokana na kodi za wapangaji kwenye nyumba yao ya urithi walioachiwa na wazazi.

Familia hiyo imeanzisha utaratibu wa kukusanya fedha hizo na kukopeshana ili kuwa na miradi mbalimbali ya kujiendeleza.

"Naomi alinijulisha jinsi mumewe alivyotia shaka mahali alipopata fedha hizo za kununulia gari, alilalamika kuwa hakutaka kumwamini kuwa alikopa fedha za familia," Marijani anaeleza.

Marijani anasema kwa nyakati tofauti amesuluhisha migogoro kadhaa ya dada yake na shemeji yake, lakini hakutarajia itafikia kugharimu uhai wa mdogo wake.


Anabainisha kuwa ingawa baadhi ya migogoro hiyo ilisababisha Naomi aliyekuwa na shahada kutoka Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere cha Dar es Salaam kuacha kazi.

Wakati wa uhai wake Naomi alifanya kazi kwenye Shirika la Utafiti la Synovate na TNS Research international na Baraza la Mtihani la Taifa( NECTA).

"Nakumbuka mdogo wangu aliwahi kulalamika mambo mengi ikiwamo kuhusu wasichana kuondoka nyumbani ghafla na kumwachia mwanaye ndipo

**INAENDELEA UK. 24**

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 8 00)



**Dondoo: Kulia**

1. Zao linalolimwa sana
7. Huunganisha kichwa na sehemu nyingine za mwili Marekani
9. Utawala
11. Furaha
13. neno la kushurutisha
15. Pimana nguvu
18. Vazi
19. Sema Naam
20. Miungu ya busara Ugiriki
24. Mji mkuu wa Tanzania
25. Mwezi wa saba
26. Mmea
27. Wafanyakazi katika Idara

**Dondoo: Chini**

1. Mtumishi wa Mungu
2. Tia watu hamu ya jambo
3. Sala
4. Mwezi wa nane katika kalenda ya Kiislamu
5. Kusokena na kutojulikana mahali kitu kilipo
8. Mji wake mkuu ni Niamey
10. Pesa ya China
11. Aina ya embe dogo jembamba
14. Maneno asemayo mtu
16. Mkahawa 17. Magonjwa
21. Mhariri 22. Heshima
23. Ukosefu wa chakula

**Jibu Na: 7**

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | F | R | I | K | A | K | U | S | I | N | I | |
| S | | A | | U | | | N | | B | A | B | A |
| H | A | R | A | K | A | | D | A | U | D | I | |
| A | | U | | U | | | A | | A | I | L | I |
| N | Y | A | S | A | L | A | N | D | | | I | |
| T | | | H | | U | | I | | K | I | S | A |
| I | S | H | A | R | A | | | | A | | I | |
| | A | | N | | N | | O | M | B | A | | |
| | M | O | G | A | D | I | S | H | U | | R | |
| | U | | W | | A | | H | I | R | I | A | |
| | R | H | E | A | | K | A | N | U | S | H | A |
| | A | | | | | | | D | | H | A | U |
| K | I | E | L | E | K | E | Z | I | | I | | A |

VVU KWA WATOTO

# Wanaokataa kusindikiza wenza kliniki ni chanzo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAZOEA ya wanaume kutofuatana na wenza wao pale wanapokuwa na ujauzito na kukataa kwenda vituo vya afya kwa ajili ya kupimwa , kumekuwa ni chanzo cha maambukizi mapya ya Virusi Vya Ukimwi (VVU), kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Zama hizi mume anatakiwa kushiriki kikamilifu na mkewe kuazia mwanzo wa mimba hadi otto anapozaliwa ili kuilinda afya ya mama na otto.

Nipashe inazungumza na vyanzo mbalimbali ili kubaini hali halisi ya tatizo hilo hasa kwa kinababa wanaokaidi kwenda pamoja na wenza wao kiliniki.

**WANAOISHI NA VVU**

Asha Haji (sio jina halisi) ni mtoto anayeishi na maambukizi aliyoyapata kutoka kwa mama ambaye sasa ni marehemu.

Anasema alikuwa akiugua kifua na homa za mara kwa mara bila ya kujua anasumbuliwa na nini lakini baada ya kufika umri wa miaka 12 alielezwa na familia yake kuwa anaishi na maambukizi na kwa muda wote analelewa na bibi yake na kwa kipindi chote anatumia dawa za kufubaza makali ya VVU.

Mzazi mwingine jina linahifadhiwa alimkinga mtoto wake baada ya kwenda hospitali kipindi cha ujauzito na kupewa ushauri, maelekezo na dawa. Anasema alipopata ujauzito mwanamume alimkimbia na kufikia hatua ya kutaka kujiua baada ya kugundulika kuwa anaishi na VVU tena ni mjamzito.

Anaeleza kuwa licha ya kwamba anaishi na maambukizi alijifungua salama na mtoto asiye na VVU na sasa ni muelimishaji mzuri kuhusu maambukizi ya VVU na amejitangaza na kujikubali hali yake.

Khamis Juma (48) na mke wake wanaishi na VVU, anaeleza kuwa mkewe akiwa na ujauzito aliambatana naye kwenda kliniki ambapo walipewa masharti maalumu ili kumwokoa mtoto asipate maambukizi.

"Wataalamu wa afya walitupa masharti tangu hatua za kumtafuta mtoto na kipindi cha kujifungua mtoto wetu, nashukuru mtoto yuko salama na sasa ana miaka 2.5", anasema Juma.

**WIZARA YA AFYA**

Takwimu za Wizara ya Afya Zanzibar, zinasema asilimia 90 ya watoto walio chini ya umri wa miaka 15 wanaoishi na VVU wameambukizwa na mama zao kutokana na kutochukua hatua za kuwakinga.

Taarifa hizo zinaonyesha kuwa, mwaka 2016 jumla ya watoto 10 walizaliwa na maambukizi ya VVU mwaka 2017 walikuwa 15, mwaka 2018 ni watoto tisa kati ya hao mmoja alifariki na wengine wanaendelea na ARVs zinazotolewa katika kliniki mbalimbali na hospitali kuu ya Mnazimmoja.

Mratibu wa huduma za kuzuia maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto kutoka Mradi Shirikishi, Ukimwi, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma Zanzibar, Khadija Abass Mohammed, anasema jumla ya watu 6,393 wanakisiwa kuwa wanaishi na maambukizi.

Kati ya hao watoto chini ya umri wa miaka 15 ni 582 na wale ambao wenye maambukizi mapya inakisiwa kuwa ni 172.

"Kati yao, inakisiwa 20 ni watoto chini ya umri wa miaka 15 huku idadi ya vifo kwa mwaka vinavyotokana na Ukimwi vinakadiriwa kufikia 115, kati ya hivyo 28 ni watoto." Anasema Khadija.

Anasema, hivi sasa hali ya maambukizi kwa Zanzibar inatisha hasa kwa ongezeko la watoto wanaozaliwa na VVU na kwamba asilimia 90 ya watoto walio chini ya umri wa miaka 15 wanaoishi na maambukizi wameyapata kwa mama zao waliokwepa kuchukua tahadhara kuwaepusha na magonjwa.




Vipimo vya damu kwa wazazi ni muhimu kufahamu namna ya kumkinga mtoto iwapo mama ameathirika ili kumwepusha na maambukizi kutoka kwa mama. **PICHA: MTANDAO.**

Anasema, watoto hao wamepata maambukizi kutokana na wazazi wao kutojijua kama wanaishi na VVU na wengine hawatumii ARVs ipasavyo. "Ili kumlinda mtoto asipate maambukizi ni vizuri kuhakikisha baba anambatana na mweza wake kwa ajili ya kupata elimu ya afya na kupata vipimo vyote ili kumkinga mtoto ," anasema mratibu huyo.

**CHANGAMOTO**

Akizungumzia changamoto zinazojitokeza katika vituo vya upimaji VVU, Khadija anasema kuwa kinamama wengi wanaopimwa hukutwa na maambukizi lakini wanaume hawana. Hata hivyo, ushiriki mdogo wa kina baba kwenye huduma hizo na unyanyapaa katika familia ni tatizo linalojitokeza.

Aidha, kuna changamoto kubwa ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto kwani wajawazito wanaacha kutumia huduma za matibabu na baadhi wanatoroka.

**TAARIFA ZA TUME**

Ofisa Uhamasishaji wa Tume ya Ukimwi (ZAC), Sihaba Saadat Haji, anasema kuanzishwa utaratibu wa wajawazito kwenda na wenza wao vituo vya afya wakati wa ujauzito ni njia moja wapo itakayoweza kupunguza maaambukizi ya VVU kwa mama kwenda kwa mtoto.

Anasema mama na mwenza wake wakiweza kwenda pamoja na kupimwa wataweza kujua afya zao na pia wataondoa udanganyifu unaofanywa na baadhi ya watu kutopima VVU wakati wanapotaka kufunga ndoa. Ofisa Saadat, anabainisha kuwa jambo la kupima afya ni la muhimu kwa wanandoa na wataweza kumkinga mtoto wao mapema kupata VVU.

"Watu tunapowajua afya zao mapema basi inakuwa rahisi kuwapa huduma ili kumkinga mtoto wao kupata maambukizi na wanapodharau ndipo idadi ya watoto wanaozaliwa na maambukizi inakuwa", alisema.

Anasema, mara nyingi baba anapokuwa na maambukizi husababisha kumuambukiza mwenza wake na baadaye hupelekea watoto kuzaliwa na VVU.

"Lengo letu ni kudhibiti maambukizi mapya ya VVU hasa kwa watoto, vijana wa rika ambao ni waathirika wakubwa wa maambukizi," anasisitiza.

**VIONGOZI WA DINI**

Askofu wa Kanisa la Anglikana Zanzibar Michel Hafidh, anasema kuwa wanaume wamekuwa wagumu kupima VVU ikilinganishwa na wanawake na kuwataka walio katika ndoa kuongozana na wake zao kwenda kupima afya mama anapokuwa mjamzito.

Aidha, Kanisa la Anglikana kwa kushirikana na shirika la afya yakinifu (Amrifu) linatekeleza mradi wa kupambana na VVU ambapo wamekua wakitoa elimu kwa waamini.

Kazi inayofanyika katika ibada na mikusanyiko mbalimbali inayoandaliwa na wadau hao. Jitihada mbalimbali zimekua zikifanyika katika kusaidia sekta ya afya kwa jamii kwa uzazi salama kwa mama na mtoto ikiwemo kuanzishwa mradi wa afya kamilifu unaopambana kupunguza maambukizi mapya ya Ukimwi.

Msimamizi wa mradi wa Afya Kamilifu Zanzibar, Dk Mohammed Hassan, anasema lengo la mradi huo ni kupunguza maambukizi mapya na kuhakikisha kwamba wale wanaoishi na VVU wanaimarika afya zao kwa kupatiwa dawa kikamilifu ili kupata vijana ambao ni wazalishaji wazuri katika taifa lao.

Anasema tasisi yao inasaidiana na serikali katika kuwajengea uwezo wataalamu wa afya ya uzazi katika vituo vya afya kwa lengo la kutoa huduma bora kwa wanajamii pamoja na kupunguza maambukizi mapya ya VVU kwa mama wajawazito na watoto Zanzibar.

Dokta Hassan anasema imefika wakati kila mmoja kuchukua jitihada za kupambana na na Ukimwi na kupunguza maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto na watu wengine ikiwa ni dhamira ya malengo ya Umoja wa Mataifa (UN) ifikapo mwaka 2020, ugonjwa huo uwe umedhibitiwa.

# Simanzi kifo cha Naomi

**INATOKA UK. 23**

akaamua kujiajiri mwenyewe kwa kuanzisha duka la dawa ili pia kumhudumia mwanaye Gadiosa,"anasema.

Marijani anabainisha kuwa nduguye pia aliwahi kulalamika kuwa mumewe alikuwa anafanya mambo ya hatari kama kuwasha jiko la gesi na kuacha gesi kusambaa ndani kwa wingi. Naomi alipofika na kuwasha ili kupika moto ulilipuka lakini alisusurika.

"Nakumbuka ulikuwa mgogoro mkubwa kwa kuwa Naomi alikasirika na kulalamika sana kuhusu kitendo hicho," Marijani anasema.

Anasema baada ya kupata taarifa za kutoweka kwa ndugu yao walipata mashaka, baada shemeji yao kuwaambia kuwa alitoweka ghafla katika mazingira yasiyoeleweka.

"Kwanza tulimuomba Mungu sana,pia tutafanya juhudi mbalimbali za kumtafuta kama wanandugu, mazingira yaliyoonekana yalisababisha tuzidi kumhisi shemeji kuwa anajua ndugu yetu alipo," alisema.

**JITIHADA**

Juhudi zilizofanywa za kumtafuta Naomi ni pamoja na kutoa matangazo kwenye mitandao ya jamii, pamoja na kushirikisha mamlaka mbalimbali.

"Tunashukuru Mungu. Shemeji amekiri mwenyewe polisi kuwa amemuua na kueleza alichofanya na jinsi ambavyo tukio la mauaji limekuwa likimtesa likimjia kwa kurudia kichwani mwake hivyo kumkosesha amani," Marijani anasema.

"Amewaeleza polisi kuwa alitumia siku tatu kuteketeza kwa moto mwili wa Naomi, ambapo alikuwa anaugeuza kama vile anachoma mishikaki, kisha kuchukua mabaki na kwenda kuyafukia kwenye shamba lao Mkuranga na kupanda mgomba," Marijani anasema.

**KUANDAA MAZISHI**

"Sasa tunasubiri uthibitisho wa vipimo vya DNA kutoka kwenye mabaki ya mwili wa ndugu yetu. Ikithibitika tutavikusanya na kuviweka kwenye jeneza jinsi vilivyo na tutamzika kwa heshima zinazostahili ili tuwe na alama ya kaburi lake,"anasema Marijani.

Mtaalam wa Saikolojia, John Ambrose maarufu kwenye mitandao ya jamii kama Johnsaikolojia anaelezea wivu wa mapenzi kwamba hujengeka kutokana na hofu na mazingira ya uhusiano ulivyoanza.

Anasema japo asingependa kuhusisha suala hilo tatizo la akili, lakini akaonya kuwa katika jamii kuna watu wenye matatizo ya afya ya akili, wengine wakikabiliwa na msongo wa mawazo na hawajajishughulisha kupata tiba.

"Hii nayo imechangia matukio ya kikatili katika jamii. Utamaduni wa mtu kuwa na matatizo ya kisaikolojia na jamii au mhusika kuyapuuzia yamechochea mambo mabaya kutokea,"anasema.

## Marekani yadungua ndege ya Iran

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amesema jeshi la maji la Marekani limetungua ndege isiyo na rubani ya Iran katika eneo la mpaka kati ya Ghuba ya Uajemi na Ghuba ya Oman.

Alisema meli ya jeshi lake "ilichukua hatua ya ulinzi" siku ya Alhamisi baada ya ndege hiyo kusogea kwa takriban mita 914 karibu na chombo hicho.

Iran haijasema chochote kuhusu hilo. Mwezi Juni, Iran iliangusha ndege ya kijeshi isiyo na rubani ya Marekani, na kusababisha hofu ya kutokea mzozo wa kijeshi.

Awali Tehran ilisema imekamata "meli ya kigeni" na wafanyakazi wake 12 siku ya Jumapili kwa kusafirisha mafuta kinyume cha sheria. Iran imekuwa ikishutumiwa na Marekani kwa kushambulia meli zake tangu mwezi Mei.Tehran mara kwa mara ilikana shutuma hizo.

Akizungumza Ikulu, Raia Trump alisema "Ninataka kuwajulisha kuhusu tukio lililotokea kwenye eneo la mpaka wa Hormuz lililohusisha meli yetu ya kijeshi.

Chombo hicho kilichukua hatua ya kujilinda dhidi ya ndege isiyo na rubani ya Iran ambayo ilikuwa karibu sana hatua iliyokuwa ikitishia usalama wa meli na waliokuwa ndani ya meli hiyo. Ndege hiyo iliharibiwa mara moja".

Ofisa wa Idara ya Ulinzi Marekani aliyenukuliwa na New York Times alisema ndege hiyo isiyokuwa na rubani imedunguliwa kwa kutumia kifaa cha kukwamisha utendaji kazi kwa njia ya umeme.

Washington awali ilisema Iran lazima iachie meli ambayo ilidai kushikiliwa na Iran. Vyombo vya habari vya Iran vililinukuu jeshi la Iran likisema kuwa meli hiyo ilikuwa imebeba lita 220,000 za mafuta. Chombo hicho kilikamatwa kusini mwa Iran, kisiwa cha Larak, Iran ilieleza. Kumekuwa na mvutano katika eneo la Ghuba tangu Marekani ilipoweka vikwazo zaidi dhidi ya sekta ya mafuta ya Iran baada ya kujiondoa kwenye mkataba wa nyuklia wa Iran wa mwaka 2015.

Marekani imeishutumu Iran kwa mashambulizi mawili dhidi ya meli za mafuta katika eneo la ghuba ya Oman mwezi Mei na Juni, shutuma ambazo Iran imezikana.

Iran pia ilidungua ndege ya kijasusi ya Marekani katika eneo la mpaka huo. Tehran imesema ndege hiyo iliingia kwenye anga lake na tukio hilo liliituma ujumbe 'wa wazi kabisa kwa Marekani.

Jeshi la Marekani lilisema ndege isiyo na rubani ilikuwa ikiruka usawa wa eneo la maji ya kimataifa tukio ambalo limeelezwa kuwa 'shambulizi la kichokozi'. BBC Uchunguzi huo, ambao Zuma alikubali kuunda katika wiki za mwisho za utawala wake, unaangazia madai ya ufisadi pamoja na matumizi ya ushawishi ambayo yalikuwapo katika utawala wake wote wa miaka tisa madarakani. **DW**

# Maelfu ya Waganda yatumikishwa kibabe

**KAMPALA,** Uganda

Uganda imelezea hofu yake kuhusu hali ya raia wa nchi hiyo wanaofanya kazi Oman ikidai kuwa huenda ni wahanga wa ulanguzi wa binadamu. Suala hilo limeangaziwa katika ripoti iliyowasilishwa bungeni jana Ijumaa ikieleza kuwa zaidi ya Waganda 40,000 wanafanya kazi Oman taifa ambalo halina makubaliano yoyote ya kibiashara na ajira za watu hao.

Serikali ya Uganda imekuwa ikijaribu kuwafikia raia wake ambao ni wahamiaji wanaofanya kazi Mashariki ya Kati baada ya kupokea simu za kutafuta msaada kutoka kwa raia hao wanaofanya kazi za ndani.

Wengi wao ni wanawake ambao wamekosa nafasi ya ajira chini mwao na kuamua kutafuta kazi katika mataifa ya Uarabuni.Lakini mpango wa ajira kwa wahamiaji umekumbwa na madai ya unyanyasaji wa kingono pamoja na dhuluma wanazopitia wafanyakazi wa ndani kutoka kwa waajiri wao.

**Kuondoa marufuku hiyo kulituwezesha kujadiliana na mataifa husika na kufikia mkataba wa kibiashara, pia ilituwezesha kuzuru mataifa hayo kubainisha kama watu wanaolalamikia visa vya unyanyasaji ni raia halisi wa Uganda.**

Wengi wao wamekuwa wakinasa kanda za video na kuzisambazwa katika mitandao ya kijamii wakiomba jamaa na marafiki wawasaidie kurudi nyumbani. Katika mkasa wa hivi karibuni mwanamke wa umri wa makamo aliyekuwa akifanya kazi Jordan, alidai kuuzwa kama mtumwa kwa Dola 3000 karibu Sh 7,000,000.

Alimpigia simu mbunge mmoja nchini Uganda ambaye baadaye aliwasilisha kisa chake katika bunge la nchi hiyo. Licha ya changamoto zinazowakabili raia wake ugenini, serikali ya Uganda imesema kuwa haitasitisha mpango wa kuwapeleka watu wake kufanya kazi nje ya nchi.

Serikali ilisema hatua ya kupiga marufuku ya muda kwa mpango huo mwezi Januari mwaka 2016 ilichangia ongezeko la matukio ya biashara haramu ya binadamu.

"Kuondoa marufuku hiyo kulituwezesha kujadiliana na mataifa husika na kufikia mkataba wa kibiashara, pia ilituwezesha kuzuru mataifa hayo kubainisha kama watu wanaolalamikia visa vya unyanyasaji ni raia halisi wa Uganda. Ukweli ni kwamba tulipochunguza walikotoka watu hao nchini Oman tulibaini kuwa ni raia wa Uganda,' aliongeza waziri huyo wa kazi.

Pia aliongeza kuwa wamefungua ofisi za kushughulikia maslahi ya wafanyakazi wa Uganda waliopo Ughaibuni na kwamba Serikali inajaribu kufanya rasmi mkataba wa ajira na Oman, ili kuhakikisha haki za Waganda wanaofanya kazi nchini humo zinalindwa.

Mkataba kama huo tayari umetiwa saini kati ya Uganda na mataifa ya Saudi Arabia, Jordan na Falme za Kiarabu (UAE).

Karibu kampuni 200 zilipewa leseni ya kuwa mawakala wa kuwatafutia kazi ng'ambo raia wa Uganda. Kampuni sita tayari zimefutiwa leseni kufuatia madai hayo ya unyanyasaji.**BBC**



Raia wa Uganda, mtumishi wa ndani huko Oman. **PICHA: BBC**

# Zuma agomea tume ya rushwa

**Johannesburg,** Afrika Kusini

WAKILI wa Rais wa zamani wa Afrika Kusini, Jacob Zuma, ameiambia tume ya uchunguzi ya madai ya ufisadi kwamba mteja wake asingeliweza kushiriki tena mahojiano na tume hiyo kwa sababu anaamini kuwa hatendewi haki kwenye mahojiano hayo.

Wakili Muzi Sikhakhane aliiambia tume hiyo ya uchunguzi mapema jana kuwa hawataendelea kushiriki vikao vya uchunguzi, kwani Zuma amekuwa muhanga wa maswali ya kuchafua na kuudhi.

Zuma alikuwa anatarajiwa kurejea katika uchunguzi wa Serikali kuhusiana na rushwa leo Ijumaa, akiwa tayari ameshahudhuria mahojiano hayo katika siku tatu za kutoa ushahidi katika uchunguzi huo wiki hii, kabla ya mawakili wake kuomba kuahirishwa kwa mahojiano hayo.

Uchunguzi huo, ambao Zuma alikubali kuunda katika wiki za mwisho za utawala wake, unaangazia madai ya ufisadi pamoja na matumizi ya ushawishi ambayo yalikuwapo katika utawala wake wote wa miaka tisa madarakani. **DW**

## HABARI MICHEZO



# LAMPARD AMHAKIKISHIA JORGINHO NAMBA

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard, amemwambia kiungo wake, Jorginho kwamba, yupo kwenye mipango ya muda mrefu na kwenye kikosi cha timu hiyo.

**Lampard ameonekana kuvutiwa na kiwango cha Jorginho, ambaye alisajiliwa na kocha Maurizio Sarri kwa pauni milioni 57 kutoka Napoli na alionekana kuwa kwenye mgogoro na mashabiki hapo Stamford Bridge msimu uliopita.**

Alizomewa na mashabiki wa Chelsea wakati alipotolewa kwenye mchezo wa Ligi ya Europa dhidi ya Malmo Februari mwaka huu, kwani alionekana kupendelewa na Sarri kwa kuchezeshwa namba ya N'Golo Kante.

Jorginho ambaye ni mzaliwa wa Brazil mwenye uraia wa Italia msimu uliopita hakuiva na mashabiki wa Chelsea kwa sababu ya kuonekana kupendelewa dhidi ya Kante.

"Jorginho alikuwa kwenye mjadala mkubwa msimu uliopita," alisema Lampard.

"Nilikuwa pale. Kama mchezaji kuna wakati mambo yanakuwa nje ya uwezo wako.

"Alipewa nafasi ya kucheza na kocha alikuwa na imani nae, pengine aliaminiwa zaidi, lakini mimi ni kocha mpya. Nina mawazo mapya. Tutacheza kwa mbinu mpya na kwa staili nyingine.

"Naweza kuwapa majukumu tofauti Jorginho au Kante au Ross Barkley au mchezaji mwingine yoyote.

"Mimi ndivyo ninavyotaka timu yangu icheze. Sitakuwa sehemu ya mjadala wa msimu uliopita. Mimi naangalia mchezaji ambaye anaweza kuisaidia timu.

"Kwa siku nilizokaa na timu hii kwenye mazoezi nimevutiwa zaidi na Jorginho na nina furaha kuwa naye kwenye kikosi changu."

## Conte akasirishwa Lukaku kuachwa

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte amekasirishwa na Inter Milan baada ya kuonekana kushindwa kumsajili Romelu Lukaku, huku sasa wakitafuta mbadala wake kwa bei nafuu, kwa mujibu wa gazeti la The Sun.

Mshambuliaji huyo wa Manchester United amekuwa akihusishwa na mpango wa kujiunga na miamba hao wa soka la Italia na ilionekana kwamba Inter walikaribia kusamjili kwa pauni milioni 75.

Lakini imeripotiwa kwamba, Inter imeshindwa kufikia bei inayotakiwa na United na sasa wanafikiria kumsajili Edinson Cavani.

Cavani ambaye ni mchezaji wa kimataifa wa Uruguay mkataba wake pale Paris Saint-Germain unamalizika kipindi kijacho cha majira ya joto, baada ya awali kuzitumia timu za Napoli na Palermo.

Mkutano wa jijini London kati ya Makamu Mwenyekiti Mtendaji wa United, Ed Woodward na Ofisa Mtendaji wa Inter, Piero Ausilio, ulishindwa kufikia muafaka juu ya ada ya Lukaku ambaye sasa majaliwa yake hayajulikani.

Inter wanataka kumchukua kwanza kwa mkopo wa miaka miwili na pauni milioni 9 na wakimsajili moja kwa moja walipe pauni milioni 54, lakini United imekataa na inataka pauni milioni 90 kwa ajili ya kumwachia mchezaji huyo waliyemsajili kutoka Everton miaka miwili iliyopita.

Lukaku alidokeza mwishoni mwa msimu uliopita kuwa anataka kuondoka na kwamba ligi ya Italia ndiyo inayomvutia zaidi kwenda kucheza.

Lakini Conte ameonekana kukasirishwa na waajiri wake hao wapya kwa kushindwa kusajili wachezaji anaowanataka na wameshindwa kutimiza ahadi yao.

Conte alihakikishiwa kwamba, klabu hiyo itafanya usajili wa nguvu kipindi hiki cha majira ya joto.

Pia aliambiwa kwamba wachezaji kama Mauro Icardi, Radja Nainggolan na Jaoa Mario watauzwa, lakini hadi sasa bado wapo klabuni hapo.



## Guardiola: Nyota City kuchagua nahodha wao



**NANJING,** China

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amesema ataawachia wachezaji wamchague nahodha ajae wa klabu hiyo baada ya kuondoka kwa Vincent Kompany aliyedumu hapo kwenye dimba la Etihad kwa miaka 11 na kwenda kuwa kocha mchezaji wa Anderlecht.

Kompany aliiongoza City katika kutwaa mataji manne ya Ligi Kuu England kwa kipindi chote alichokaa hapo.

David Silva ambaye ndiye mchezaji anayefuata kwa kucheza hapo kwa muda mrefu zaidi baada ya mchezaji huyo wa Ubelgiji, ndio aliyekabidhiwa kitambaa cha unahodha, na pia alikuwa nahodha wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya West Ham United kwenye mchezo wa kirafiki uliopigwa hapa Nanjing Jumanne.

Hata hivyo, bosi huyo wa City hajafanya uamuzi wowote juu ya kumteua nahodha mpya na wa kudumu wa timu hiyo.

"Watachagua nahodha tutakapokuwa wote pamoja," alisema Guardiola akizungumzia nahodha mpya.

Kwa upande wake, Kevin De Bruyne alisema kwamba yeye atajisikia furaha kuwa nahodha wa timu hiyo kama akipata nafasi hiyo.

"Kama timu itanitaka mimi kuwa nahodha, au klabu itanipa nafasi, nitakubali, lakini nafikiri hicho ni kitu muhimu na ambacho kila mchezaji angependa kupewa nafasi hiyo."

City itaanza kutetea taji lake la Ligi Kuu Agosti 10 kwa kucheza na West Ham.

## HABARI MICHEZO

# Hudson-Odoi kusaini miaka mitano Chelsea

**LONDON,** England

KINDA Callum Hudson-Odoi amefikia makubaliano na Chelsea na sasa anajiandaa kusaini mkataba mpya wa miaka mitano chini ya kocha, Frank Lampard.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 18 alikuwa akiwaniwa na Bayern Munich, ambao walitoa ofa ya pauni milioni 35 kwa ajili ya kumsajili Januari, lakini Chelsea waliikataa.

Lakini sasa Hudson-Odoi amekubali kubakia hapo Stamford Bridge chini ya kocha mpya, Lampard.

Hudson-Odoi, ambaye alianza kuichezea timu ya taifa ya England dhidi ya Jamhuri ya Czech Machi mwaka huu, atakuwa akilipwa mshahara wa pauni 100,000 kwa wiki.

Mkataba wa sasa wa Hudson-Odoi ulikuwa imalizike mwakani na ilioneaka kama hataki kubakia katika timu hiyo.

Kocha, Maurizio Sarri, hakuwa tayari kumtumia Hudson-Odoi hali ambayo ilisababisha wawakilishi wake kutoifurahishwa na walimshawishi kuondoka.

Na sasa Lampard amebainisha kwamba ana mipango na mchezaji huyo na kwamba yupo kwenye mipango yake ya baadae.

Mapema wiki iliyopita, Lampard alibainisha kwamba angefanya mazungumzo binafsi na Hudson-Odoi ili kuhakikisha anabakia klabuni hapo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyoripotiwa na gazeti la Daily Mail, Hudson-Odoi sasa atasaini mkataba mpya mapema wiki ijayo.






# POCHETTINO ALIPANGA KUONDOKA SPURS

**SINGAPORE,** Singapore

MAURICIO Pochettino amethibitisha kuwa angeondoka Tottenham kama wangeshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Kabla ya mchezo wa pili wa nusu fainali, ambapo Spurs walipindua matokeo dhidi ya Ajax na kutinga fainali, kocha huyo raia wa Argentina alitoa kauli kwamba anafikiria kuondoka.

Na sasa akizungumza katika kambi ya mazoezi ya Tottenham ya kujiandaa na msimu mpya nchini Singapore, Pochettino amebainisha kwamba angeweza kuondoka kama wasingefungwa na Liverpool mabao 2-0.

"Pengine kama yangekuwa matokeo tofauti, ningefikiria kuondoka," alisema Pochettino.

"Kubeba Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwangu ilikuwa ni kigezo kizuri cha kwenda kuangalia changamoto nyingine katika ngazi tofauti, lakini matokeo yale yakanifanya nibadili mawazo," alisema.

"Lakini kwa sasa nina mawazo tofauti, ingawa kwa hapo baadaye chochote kinaweza kutokea."

Pochettino, mara kwa mara alikuwa akihusishwa na kutakiwa na klabu za Manchester United na Real Madrid, lakini baadaye alikubali kubakia kwa miamba hao wa London Kaskazini.

# *Perez: Hatuwezi kumsajili Pogba*

**MADRID,** Hispania

RAIS wa Real Madrid, Florentino Perez amemthibitishia kocha, Zinedine Zidane kwamba itakuwa ni vigumu kumsajili kiungo wa Manchester United, Paul Pogba kipindi hiki cha majira ya joto.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia amekuwa akihusishwa na mpango wa kutua pale Santiago Bernabeu kipindi hiki cha majira ya joto, huku United wakiweka ngumu kumwachia.


Pogba mwenyewe ameshabainisha wazi kwamba, anataka kuondoka hapo United kwa sababu anataka kutafuta changamoto mpya.

Hata hivyo, gazeti la Marca limemnukuu rais Perez kwamba uwezekano wa kumsajili Pogba kipindi hiki cha majira ya joto haupo.


Perez alifanya mkutano na kocha, Zidane na Mkurugenzi, Jose Angel Sanchez kwenye hotel ya Mont wiki iliyopita kwa ajili ya kujadili mustakabali wa usajili kwa kipindi hiki cha majira ya joto.

Katika mkutano huo, Perez alibainisha wazi kwamba United hawako tayari kumwachia Pogba na hivyo uwezekano wa kumsajili kipindi hiki cha majira ya joto ni ngumu.

Madrid iliamini kwamba, Pogba angeweza kulazimisha uhamisho wake kuondoka pale Old Trafford, lakini sasa Perez amekata tamaa.



# DONDOO SOKA MAGAZETI ULAYA




# USAJILI WA NEYMAR KUITINGISHA BARCA

●●● Klabu hiyo ya Hispania yajipanga kutoa pauni milioni 90 na wachezaji wawili...

**BARCELONA,** Hispania

UONGOZI wa Barcelona umeripotiwa umewasilisha ofa kwa Paris Saint-Germain ya pauni milioni 90 pamoja na wachezaji wawili ili kumsajili mshambuliaji wake wa zamani Mbrazil, Neymar.

**Klabu hiyo ya Hispania imewapa mabingwa hao wa Ligi Kuu Ufaransa, orodha ya majina ya wachezaji sita ili wachague wawili kati ya hao, ikiwa ni sehemu ya ofa ya usajili huo.**

Nyota ambao wameorodhesha kuhusika katika usajili huo ni pamoja na Philippe Coutinho, Ousmane Dembele, Ivan Rakitic, Nelson Semedo na Malcom, wakati mchezaji anayekamilisha idadi ya nyota sita kukamilika haijafahamika, imeandika Sky Sports.

Neymar ameweka wazi nia yake ya kutaka kuondoka PSG na klabu hiyo ya Hispania imeonyesha wazi nia yake ya kumsajili huku pia ikiwa tayari kuongeza wachezaji wengine ili kukamilisha thamani ya Mbrazil huyo.

PSG sasa imeshakubali uamuzi uliofanywa na mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 27 wa kuondoka klabuni hapo lakini unahitaji kuona wanalipwa kiasi cha fedha cha pauni milioni 198, ambacho wao walitumia mwaka 2017 wakati wanamsajili na kuweka rekodi ya dunia.

Hata hivyo, Barca haiko tayari kulipa kiasi hicho cha fedha kilichotajwa na inataka kuona malipo ya mchezaji huyo yanalipwa hadi Julai mwakani.

Baada ya kukamilisha usajili wa Antoine Griezmann, ambao umewagharimu kiasi cha pauni milioni 108, klabu hiyo ya Katalunya iliamua kuwasilisha kiasi kidogo cha ada ya kumsajili mchezaji huyo ikijumuisha na wachezaji wawili ili kuhakikisha inajiweka mahali salama na kanuni za matumizi ya fedha zilizopo.

Barcelona inafahamu wazi kwamba endapo itavuka kiwango cha matumizi ya fedha, itakumbana na adhabu ya kufungiwa.

Neymar alirejea jijini Paris katika mazoezi ya maandalizi ya msimu mpya Jumatatu baada ya kudharau wito uliotolewa na uongozi wa timu hiyo kuwasili kambini mapema, huku akidaiwa alikuwa nchini kwao Praia Grande akicheza mechi za mashindano zilizohusisha timu za wachezaji watano watano.

Nyota huyo wa zamani wa Santos, anatarajia kuendelea kusubiri kuona kama ofa yake itafikia mwisho wakati wawakilishi wa klabu hizo mbili watakapokamilisha mazungumzo ambayo yanaweza kumfanya Mbrazil huyo akarejea Hispania.

## ZISIKUPITE

### PEREZ AMPANGA ZIDANE

RAIS wa Real Madrid, Florentino Perez anajaribu kumshawishi Kocha, Zinedine Zidane kusitisha uamuzi wake wa kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa na Manchester United, Paul Pogba (26), na badala yake kujipanga kumtumia Gareth Bale kwa sababu bado klabu hiyo inahaha kumuuza mshambuliaji huyo wa Wales mwenye umri wa miaka 30. ***(Independent)***

### LUKAKU MAMBO MAGUMU

MCHAKATO wa straika wa United, Romelu Lukaku kujiunga na Inter Milan umeanza kuingia dosari baada ya klabu hiyo ya Italia kuanza kusita kiasi cha dau la pauni milioni 75 ambacho kimetajwa ili kumnasa Mbelgiji huyo mwenye umri wa miaka 26. ***(Sun)***

### CELSO ATAKIWA SPURS

MABOSI wa Tottenham wanajiandaa kuvunja rekodi ya uhamisho kwa mara ya pili kwa kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Argentina na Real Betis, Giovani lo Celso kwa kuwasilisha ofa ya pauni milioni 70. ***(Mirror)***

### PSG, SCHALKE VITANI

PARIS St-Germain na Schalke zimeonyesha kumsajili beki wa Timu ya Taifa ya England, Danny Rose ambaye anaichezea Tottenham, na thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 20. ***(Sky Sports)***

### BRUCE, LONGSTAFF KUTETA

KOCHA wa New Newcastle, Steve Bruce anatarajia kufanya mazungumzo na Sean Longstaff (21), ili kumshawishi kiungo huyo raia wa England akatae ofa ya kujiunga Manchester United. ***(Sky Sports)***

### ARSENAL: CEBALLOS NI WETU

ARSENAL inamatumaini makubwa kuwa itafanikisha mchakato wa kumsajili kwa mkopo kiungo wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Hispania, Dani Ceballos ambaye ana umri wa miaka 22. ***(Goal)***

### ZAHA: NATAKA KUONDOKA

MSHAMBULIAJI wa Ivory Coast, Wilfried Zaha, ameieleza Crystal Palace kuwa anataka kuondoka klabuni hapo, Arsenal inatajwa kumwania mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. ***(Sky Sports)***

### HUDSON-ODOI KITAELEWEKA

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Timu ya Taifa ya England, Callum Hudson-Odoi (18), anatarajia kukamilisha mchakato wa kusaini mkataba mpya na klabu hiyo ambao utamfanya awe analipwa mshahara wa pauni 100,000 kwa wiki. ***(Mail)***

### JOELINTON ANUKIA NEWCASTLE

KLABU ya Hoffenheim imethibitisha kuwa straika, Joelinton (22), yuko katika hatua za mwisho za kukamilisha mazungumzo ya kujiunga na Ligi Kuu England na Newcastle United inaamini itakamilisha mchakato wa kumsajili Mbrazil huyo kwa dau litakaloweka rekodi. ***(Chronicle Live)***

### RODGERS AMPONGEZA MAGUIRE

KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers, amesema kuwa amefurahishwa na hali ya ukomavu iliyoonyeshwa na Harry Maguire na kukiri kwamba "hajawahi kupata wasiwasi" kuhusu beki huyo wa kati kuwaniwa na Manchester United. ***(Independent)***

HABARI MICHEZO

## UDSM yaviita vyama vya michezo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BEKI tegemeo wa Timu ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes), Mohammed Mmanga, amejiunga rasmi na timu ya Polisi Tanzania ambayo inashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara akitokea Polisi ya visiwani hapa, imefahamika.

Polisi Tanzania na Namungo ndio timu mbili zilizopanda daraja na zimeanza kujiimarisha kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Bara unaotarajiwa kufanyika kuanzia Agosti 23 mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Polisi Zanzibar, Nassor Salum, alisema kuwa Mmanga amekamilisha mchakato wa kujiunga na Polisi Tanzania na wanaamini mchango wake utasaidia kuimarisha safu yao ya ulinzi wa timu hiyo iliyopanda daraja msimu huu.

Salum alisema kuwa Mmanga alikuwa ni mmoja wa wachezaji muhimu katika kikosi chake, lakini walelazimika kumruhusu kuhamia Bara ili akatafute changamoto mpya.

"Tayari washamalizana kila kitu na mabosi wa Polisi Tanzania, napenda kusema kuwa msimu mpya wa Ligi Kuu Bara utakapoanza, Mmanga atakuwa sehemu ya kikosi hicho cha Polisi Tanzania," alisema Salum.

Aliongeza kuwa kuondoka kwa beki huyo kumeacha pengo katika timu yake, hasa baada ya kufanikiwa kukijenga na vizuri ikilinganishwa na msimu uliopita.

## Songea Girls wang'ara Majimaji Selebuka

**Na Renatha Msungu**

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Songea wameacha alama ya kipekee baada ya kukomba medali zote kwenye Shindano la Mdahalo kwa Shule za Sekondari linaloratibiwa na Taasisi ya Songea-Mississippi (So-Mi), kupitia tamasha la Majimaji Selebuka.

Tamasha hilo ambalo hufanyika kwa wiki nzima, mwaka huu ilikuwa ni msimu wake wa tano tangu lianzishwe huku kipengele cha mdahalo kwa Shule za Sekondari kikiongoza kwa ushindani mkali kwa shule kupokezana ubingwa.

Katika mdahalo wa mwaka huu, mada ilikuwa inasema: 'Fedha Ndiyo Msingi wa Afya Bora?.' Ambapo kila shule ilikuwa inawakilishwa na wanafunzi wawili, mmoja akiunga mkono mada na mwingine akipinga.

Shule hiyo iliibuka kinara baada ya kujikusanyia alama 874 kati ya shule nne zilizoingia hatua ya fainali katika shindano hilo lililoshirikisha shule 16 huku nafasi ya pili ikienda kwa Shule ya Msamala iliyopata alama 802 wakati Daora ya Dar es Salaam iliyoshiriki kama mwalikwa, ilishika nafasi ya tatu kwa alama 779.

# STRAIKA AIPELEKA MTIBWA SUGAR LIGI YA MABINGWA

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI akiwa katika maandalizi ya kujiandaa na msimu mpya wa mwaka 2019/20, mshambuliaji wa Mtibwa Sugar ya Manungu, Turiani mkoani Morogoro, Mtibwa Sugar, Stahimili Mbonde, ametoa siri ya yeye kutofanya vizuri msimu uliopita wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Akizungumza na Nipashe jana, Mbonde, alisema kuwa sababu iliyomfanya asifanye vizuri ni kutoelewana vizuri na benchi la ufundi la timu hiyo.**

Mbonde alisema kuwa licha ya kujituma vema kwenye mazoezi ya timu hiyo, muda mrefu hakuwa na wakati mzuri na makocha wa timu hiyo.

"Msimu uliopita sikufanya vizuri kama ilivyo kawaida yangu, sababu kubwa iliyokuwa inanikwamisha ni kutoelewana na viongozi, kwa kifupi nilikuwa na matatizo na viongozi wangu," alisema Mbonde.

Hata hivyo beki huyo wa zamani wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), alisema tayari matatizo yaliyokuwa yanamkwamisha yamemalizika, baada ya kukaa pamoja na viongozi na kuyamaliza yale yaliyokuwa yanamkwamisha.

"Nimejiandaa kurejea nikiwa imara zaidi, msimu ujao nitaonekana uwanjani kama kawaida, tayari tumeshayamaliza, ninaomba mashabiki wangu wasiwe na wasiwasi," Mbonde alisema.

Aliongeza kuwa wachezaji wote wa Mtibwa Sugar wanajifua vema kwa ajili ya kujiandaa kukabiliana na ushindani ambao watakutana nao katika msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara, pamoja na mashindano ya Kombe la FA.

"Tunataka kufanya vizuri katika msimu ujao, mimi binafsi ninaahidi kurudi nikiwa na ushindani mkubwa," aliongeza mshambuliaji huyo.

Alisema kuwa wachezaji wote wa timu hiyo wamejiandaa kupata mafanikio kwa kupambana kutwaa ubingwa wa ligi au Kombe la FA ili wapate tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa mwakani.



Mshambuliaji mpya wa Yanga, Issa Bigirimana (kulia), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Moro Kids katika mechi ya kirafiki iliyochezwa mkoani Morogoro jana. Yanga ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

## *Mbio za magari kufanyika Iringa*

**Na Friday Simbaya,** Iringa

MADEREVA 17 kutoka sehemu mbalimbali wamethibitisha kushiriki katika mashindano ya mbio za magari za Mkwawa (Mkwawa Rally 2019), ambazo zimepangwa kufanyika leo na kesho mkoani hapa, imeelezwa.

Mbio hizo zimeandaliwa na Klabu ya Michezo ya Magari ya Iringa (IMSC) na kudhaminiwa na kampuni mbalimbali huku wazalishaji wa Maji ya Mkwawa wakiwa ndio wadhamini wakuu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Kamati ya mashindano hayo, Amjad Khan, alisema maandalizi ya mashindano hayo yamekamilika na wanatarajia madereva wote waliothibitisha kushiriki mbio hizo watatimiza ndoto zao.

Khan alisema kuwa lengo la mashindano hayo ni kuwahamasisha vijana na kupenda michezo na hasa mbio za magari na vile vile kutumia michuano hiyo kuutangaza Mkoa wa Iringa.

Naye Mwakilishi wa Maji ya Mkwawa, Maria Mhina, alisema wameendelea kuudhamini mchezo huo kwa mwaka watatu mfululizo ili kuendelea kuwahamasisha vijana na watu wengine kupenda michezo hasa mbio za magari.

Mhina alisema kuwa wanawaomba wakazi wa mkoa huo kujitokeza kwa wingi leo na kesho kushuhudia madereva wanavyochuana katika mbio hizo ambazo hufanyika kila mwaka.



# Michezo

Jumamosi Julai 20, 2019

Nipashe




Usajili wa Neymar kuitingisha Barca UKURASA 30



Wachezaji wa Simba Meddie Kagere (kushoto) na Gadiel Michael, wakiwa kwenye maandalizi ya msimu mpya yanayoendelea katika mji wa Rustenburg, Afrika Kusini. **PICHA: SIMBA SC**

## Yanga yaendeleza makali Morogoro

**Na Shufaa Lyimo**

YANGA imeendelea kufanya vema katika mechi zake za kirafiki baada ya kupata ushindi wa pili mfululizo kwa kuwafunga Moro Kids mabao 2-0 katika mchezo wa kirafiki uliochezwa jana kwenye Uwanja wa Highland Parks mkoani Morogoro.

Mabao ya Yanga katika mchezo huo wa jana yalifungwa na Mganda Juma Balinya aliyefunga kwa njia ya penalti huku lingine likipachikwa na Paul Godfrey.

Mratibu wa Yanga, Hafidh Saleh, alisema jana kuwa wachezaji wa timu hiyo wameendelea kuonyesha ushindani katika mchezo huo ambao Kocha, Noel Mwandila, aliendelea kutoa nafasi mbalimbali kwa nyota wa mabingwa hao wa historia.

"Mechi ilikuwa nzuri, wachezaji wameendelea kuonyesha ukomavu na kila mmoja anataka kujihakikisha nafasi kwenye kikosi cha kwanza, wanataka kuwa imara kabla ya Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera hajafika kambini hapo," alisema Saleh.

Katika mchezo wa kwanza wa kirafiki uliochezwa mkoani humo, Yanga ilipata ushindi wa mabao 10-1 dhidi ya Tanzanite Academy.

# Kidao: Stars itafuzu Afcon

**Na Mwandishi Wetu**

## ●●● Asema tukijipanga na kufanya maandalizi bora tutaenda Cameroon...

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limesema kuwa Timu ya Taifa (Taifa Stars), inaweza kukata tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon 2021), zitakazofanyika nchini Cameroon endapo tutajipanga na kujiandaa vema na michuano hiyo.

**Taifa Stars iliyoshiriki fainali za Afcon mwaka huu huko Misri, ilitolewa katika hatua ya makundi baada ya kufungwa mechi zote tatu ilizocheza za Kundi C dhidi ya Senegal, Kenya na Algeria.**

Katika kampeni ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali hizo zijazo, Taifa Stars imepangwa katika Kundi J pamoja na timu za Tunisia, Libya na Equatorial Guinea. Libya na Equatorial Guinea, hazikushiriki kwenye fainali za mwaka huu ambazo zilimalizika rasmi jana.

Mechi za kwanza za kuwania tiketi ya kushiriki fainali hizo zitachezwa kati ya Agosti 7 na 15 mwaka huu wakati marudiano yatakuwa ni kati ya Novemba 11 na 19 mwaka huu huku za pili zikichezwa kati ya Agosti 31 hadi Septemba 8 mwakani na marudiano yakipangwa kufanyika kati ya Oktoba 3 hadi 15 mwakani.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao, alisema kuwa kundi hilo la Taifa Stars ni gumu, lakini katika dunia ya soka ya sasa hakuna timu nyepesi.

Kidao alisema kuwa mpira wa miguu sasa umebadilika na kinachotakiwa ni timu kuandaliwa vema ili iweze kupambana katika mechi zake zote za nyumbani na ugenini.

"Ni moja ya makundi magumu, lakini mpira umebadilika sana,tukijipanga vizuri kwa kufanya maandalizi mazuri, tunaamini tutafuzu," alisema Kidao, mchezaji wa zamani wa Simba na Mwenyekiti aliyejiuzulu wa Chama cha Makocha Tanzania (TAFCA).

Katibu huyo alisema pia shirikisho hilo liko katika hatua za mwisho za mazungumzo na mdhamini mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Mdhamini wa ligi ameshapatikana, tupo katika hatua za mwisho za mazungumzo kabla ya kusaini mkataba," Kidao alisema katika mahojiano maalumu.

Aliongeza kuwa changamoto ya mabadiliko ya ratiba ya Ligi Kuu Bara iliyotokea mwaka jana na kusababisha kuwa na mechi nyingi za viporo, Kidao alisema kuwa ilitokana na mabadiliko yaliyofanywa katika kalenda ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), ambayo ilibadili mwanzo wa kuanza msimu katika mashindano yake ya Ligi ya Mabingwa na Kombe na Shirikisho.

Kuhusu sherehe za tuzo, kiongozi huyo alisema kuwa shirikisho linaendelea kufanyia kazi na zimechelewa kutolewa kwa sababu ya changamoto ya kukosa mdhamini mkuu wa ligi hiyo kwa msimu uliopita.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042